**MUSWADA** wabainisha ajira 15,000 katika bomba mafuta ghafi

UKURASA 4



**RAIS** Samia amlilia Mhandisi Mfugale

UKURASA 5




UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Julai 1, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580628

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710


# SAMAKI WA MAGUFULI

**SERIKALI** yakuna kichwa mtihani kumlipa aliyeshinda kesi... *Endelea Ukurasa 2*



Meli ya Tawaliq 1 iliyokamatwa mwezi Machi, 2009 ikiwa na tani za samaki aina ya Jodari, iliyowavua katika Bahari ya Hindi ndani ya Ukanda wa Kiuchumi wa Tanzania (EEZ), wakati ilipoanza kuzama mahala ilipoegeshwa upande wa Kigamboni, mkoani Dar es Salaam. Picha nyingine; meli hiyo ikionekana kidogo jana, baada ya sehemu kubwa kuzama kabisa. **PICHA: MIRAJI MSALA/MAKTABA**

## Rukhsa kuanzia nyungu nyumbani kisha hospitalini

UKURASA 2

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**UJUMBE ULIOMO KATIKA BARUA YA RAIS BUNGENI**
RAIS Samia Suluhu Hassan, ameeleza namna anavyovutiwa na Bunge la 12 kuwa kitovu cha demokrasia barani Afrika, jambo ambalo limesababisha Tanzania...

**UKURASA WA 5**

**MAGEREZA YAJA NA MKAKATI KUPUNGUZA MSONGAMANO**
JESHI la Magereza limesema linaanza utekelezaji mkakati wa ujenzi wa magereza mapya katika wilaya 46 nchini, ili kuondokana na uhaba, jambo linalosababisha...

**UKURASA WA 8**

**BIL. 2.3/- KUTOA VIFAA, ELIMU YA COVID-19 KWENYE BAA**
SHILINGI bilioni 2.3 zinatarajiwa kutumika katika mpango maalumu wa kutoa elimu, kusambaza vifaa ikiwamo vitakasa mikono...


## MAJALIWA AWAONYA MA-RC KUENDEKEZA KULA, WALINZI BINAFSI

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA YATISHWA NA MORRISON, MIQUISSONE UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

# Rukhsa kuanzia nyungu nyumbani kisha hospitalini

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imewaruhusu watu wanaojihisi kuugua corona watumie 'nyungu' huku wakiwa na hatua zaidi ya kuhamia hospitalini.

Mkurugenzi wa Tiba wa Wizara hiyo, Dk. Leonard Subi, aliiambia Nipashe juzi kuwa hatua ya kuwahi hospitalini ina tafsiri pana kitabibu, kwa sababu inamnusuru mgonjwa kabla hajafikia hatua mbaya, ambayo kimsingi si salama kwa anayeugua.

"Unapoonyesha una dalili usipoteze muda, ukija hospitali umechelewa inakuwa ni ngumu sana kukurudisha katika hali yako, tuliona katika wimbi la pili watu wanakuja kwa kuchelewa.

"Usikae tu nyumbani na kupiga nyungu, piga nyungu ukiwa na afya njema, lakini ukiona kama umeanza kupata dalili tafadhali sana fika usisubiri mpaka ushindwe kupumua," alisema.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake mkoani Dodoma, Dk. Subi, alisema nchini kuna dawa za asili na wanaziamini, lakini zinategemea na wakati wa kutumia.

"Dawa ya asili lazima ujue unaitumia wakati gani na inakusaidiaje, using'ang'anize wakati kuna wataalamu na wanasayansi wapo. Tanzania tumesema tiba asili tutaendelea nazo, lakini kuzifanyia utafiti tujue tiba gani ni nzuri na inaleta matunda gani," alisisitiza Dk. Subi.

Anafafanua zaidi kuwa, magonjwa mengi ya virusi huwa hayana dawa ya moja kwa moja na kwamba nyingi ni kinga yako ya mwili inavyoweza kukusaidia kukabiliana na magonjwa.

"Lakini tunasisitiza watu kuwahi katika vituo vya kutolea huduma, watu walikuwa wakichelewa. Tunaendelea kusisitiza watu wawahi katika vituo vya afya kupata huduma na wataalamu wa afya siyo kwingineko, wataalamu kila siku wanaonana na wagonjwa, kwa hiyo tusiangalie mitandao ya kijamii ikaanza kukufundisha ukapotea," alionya.

Alisema wanaendelea kuimarisha wataalamu wao ili kuhakikisha wanakuwa imara katika mapambano dhidi ya ugonjwa huu.

Alisema suala hilo linaenda sambamba na kuhakikisha katika maeneo yote muhimu kama vituo vyote vya huduma kwenye maeneo ya mipakani.

"Tunakuwa na rasilimali ya kutosha katika kukabiliana na ugonjwa huu, lakini tunashukuru kwamba utaratibu huu siyo katika ngazi ya taifa tu pia katika ngazi ya mikoa," alisema.

Dk. Subi alisisitiza maeneo yote ya umma na binafsi katika makanisa na misikiti watu watumie vipukusi ili kujikinga na kuenea kwa maradhi hayo.

*Usikose kufuatilia mahojiano maalum ya Nipashe na Dk. Subi katika toleo letu la kesho.



Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, akizungumza katika hafla ya kuwatambua wazalishaji bora wa maziwa ya ng'ombe, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mtihani samaki wa Magufuli

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI upande wa utetezi ukisubiri kutekelezwa kwa hukumu ya serikali kulipa fidia ya mabilioni ya shilingi kutokana na kukamata meli ya Tawariq 1 iliyokuwa na samaki mwaka 2009, maarufu Samaki wa Magufuli, serikali imesema inafikiria kuiuza meli hiyo kama chuma chakavu.

Meli hiyo iliyodaiwa kuwa na thamani ya Dola za Marekani 2,300,000 na samaki wenye thamani ya Sh. bilioni 2.074, ilikamatwa Machi 8, 2009 na boti ya askari wa doria wa Tanzania, Afrika Kusini na Botswana. Ilidaiwa leseni waliyokuwa nayo ilikuwa imemaliza muda wake Desemba Mosi, 2008.

Wiki iliyopita, Nipashe ilimtafuta Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Palamagamba Kabudi, kuzungumzia suala hilo na alisisitiza utekelezaji wa hukumu iliyotolewa na mahakama unafanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Akizungumza na Nipashe kuhusu suala hilo jana, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema:

"Ile meli bado iko pale ilipowekwa na 'actually' imeziba nafasi. Sisi tulianza kufikiria tuiuze kama chuma chakavu kwa sababu imeziba nafasi ambayo meli zingine zinaweza kuwekwa pale.

"Kwa ufafanuzi zaidi wa suala lenyewe, ninaomba nipate muda zaidi nione hatima ya serikali kupata fedha kwa maana tupige bei kama chuma chakavu ile meli iachie nafasi. Kwa hiyo, lile suala ni kama limeisha lakini bado halijaisha."

Machi 2017 kampuni ya uwakili iliyokuwa inawatetea 'Wachina wa Samaki wa Magufuli', ilitarajiwa kwenda Mahakama ya Kimataifa ya Bahari kujua hatima ya madai yao ya meli ya Tawariq 1 yenye thamani ya Dola za Marekani 2,300,000 na zaidi ya Sh. bilioni mbili za samaki endapo hukumu haitatekelezeka.

Kampuni hiyo ilikusudia kuchukua uamuzi huo endapo hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Agosti, mwaka 2014 haitatekelezeka.

Hatua huyo imefikiwa kutokana na uamuzi uliotolewa na Mahakama Kuu kwamba suala hilo lirudi Mahakama ya Kisutu ambako amri ya kurejeshewa vitu hivyo ilitolewa.

**MAHAKAMA KUU**

Uamuzi wa kuwataka wadai kudai utekelezaji wa hukumu ya Mahakama ya Kisutu ulitolewa na Jaji Munisi kutokana na hoja za Jamhuri.

Aliyekuwa Wakili wa Serikali Mkuu, Timon Vitalis katika hoja za pingamizi alidai Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam haiwezi kusikiliza maombi ya 'Wachina wa Samaki wa Magufuli' ya kutaka kurejeshewa meli yao iliyozama na samaki kwa sababu amri ya kurejeshewa ilitolewa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Upande huo wa Jamhuri ulidai mwombaji katika maombi hayo ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Tawariq, Said Mohammed, hana sifa ya kukabidhiwa mali hiyo, hivyo waliomba mahakama itupilie mbali maombi ya kutaka kurejeshwa meli ya Tawariq 1 na zaidi ya Sh. bilioni mbili za tani 296.3 za samaki.

Maombi hayo yalitokana na kesi iliyokuwa inawakabili Nahodha wa Meli, Hsu Chin Tai na Wakala wa Meli ya Tawaliq 1, Zhao Hanquing.

Wachina hao walikuwa wakikabiliwa na mashtaka ya uvuvi haramu katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari ya Tanzania.

Vitalis alidai haiwezekani maombi hayo yapelekwe Mahakama Kuu kwa sababu Mahakama ya Kisutu ilishaamuru mali akabidhiwe mshtakiwa wa kwanza aliyekuwa kapteni wa meli hiyo.

Alidai Mahakama ya Rufani ilishafuta mwenendo wa kesi ya msingi wa Mahakama Kuu, hivyo maombi hayo ni batili na hayawezi kusikilizwa na kutolewa amri mbili katika mahakama mbili zinazohusu kitu kimoja.

Mdai katika maombi alikuwa ni mwajiri wa Wachina hao, Said Mohammed, akiwakilishwa na Mawakili Kapteni Ibrahim Bendera na John Mapinduzi.

Mawakili hao walifungua kesi hiyo kwa hati ya dharura dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), wakidai Meli ya Tawariq 1 yenye thamani ya Dola za Marekani 2,300,000 na Sh. 2,074,249,000 ambazo ni gharama za samaki zilizofanyiwa uthamini Oktoba Mosi 2009.

Meli hiyo ilifanyiwa uthamini mwaka 2008 na kuonyesha kwamba thamani yake ni Dola 2,300,000. Ripoti hiyo ilitolewa na Kampuni ya Cambodia Shipping Services Ltd.

Akijibu hoja za Jamhuri, Kapten Bendera alidai kuwa waliwasilisha maombi hayo mahakamani hapo kwa sababu Mahakama ya Kisutu ilikataa kurejesha mali hizo kwa mshtakiwa wa kwanza.

Kapteni Bendera alidai waliwasilisha maombi hayo Mahakama Kuu kwa sababu vielelezo vilitolewa katika mahakama hiyo wakati wa usikilizwaji wa kesi ya msingi.

**MAHAKAMA YA KISUTU**

Agosti mwaka 2014, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu iliwaachia huru washtakiwa katika kesi ya 'Samaki wa Magufuli' na kuamuru Jamhuri iwarejeshee vitu vyao, ikiwamo meli ya Tawariq 1.

Washtakiwa hao waliachiwa kwa mara ya pili -- mara ya kwanza waliachiwa na Mahakama ya Rufani Machi 28, 2014, lakini walikamatwa tena na kushtakiwa upya kwa mashtaka hayo hayo yaliyofutwa.

Septemba Mosi, 2014, wadai waliwasilisha barua mbele ya Msajili wa Mahakama hiyo wakiomba mahakama iwarejeshee vielelezo vilivyotolewa mahakamani wakati kesi namba 38 ya mwaka 2009 mbele ya Jaji Radhia Sheikh ilipoisikilizwa.

Barua hiyo ilivitaja vielelezo hivyo kuwa ni meli ya uvuvi Tawariq 1 pamoja na Sh. 2,074,249,000 za tani 296.3 za samaki walizokutwa nazo washtakiwa ambavyo vilitolewa Oktoba Mosi, 2009 mbele ya Jaji Sheikh.

**UFAFANUZI KISHERIA**

Jana, Wakili Reuben Simwanza aliiambia Nipashe kuwa endapo upande wa Jamhuri unashindwa kutekeleza amri ya mahakama ya kurejesha vielelezo kwa mshtakiwa ama washtakiwa walioshinda kesi, hatua ya kwanza ya kuchukua ni kuandika barua kwa 'incharge' wa mahakama husika.

Kama barua imeandikwa kukumbushia na hakuna utekelezaji wowote, wahusika ama wadai wa vielelezo hivyo wanapaswa kuchukua hatua ya pili ambayo ni kuishtaki Jamhuri ama Ofisi ya DPP kwa kukaidi amri ya mahakama.

## HABARI KITAIFA

# Ujumbe uliomo katika barua ya Rais Bungeni

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameeleza namna anavyovutiwa na Bunge la 12 kuwa kitovu cha demokrasia barani Afrika, jambo ambalo limesababisha Tanzania ichaguliwe kuwa makao makuu ya Sekretarieti ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola Barani Afrika.

Aidha, amelipongeza Bunge hilo kwa kupiga hatua kubwa ya kuongeza uwakilishi wa makundi ya wanawake na vijana, akisema huo ndio mwelekeo mzuri katika kuimarisha uwiano wa uwakilishi kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, jana aliwasomea wabunge barua hiyo ya Rais Samia, baada ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kumaliza kusoma hotuba ya kuahirisha Bunge.

Wakati Ndugai anasoma jana ilikuwa Siku ya Maadhimisho ya Mabunge Duniani, alisema: "Mheshimiwa Rais anasema napenda kutumia fursa hii kutuma salamu za pongezi kwako Mheshimiwa Spika, kupitia kwa Bunge letu tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuisimamia serikali.

"Mheshimiwa Rais anatupongeza wote kwa kujitoa kwetu katika kuwawakilisha wananchi kupitia hoja na mapendekezo yanayolenga kuboresha maisha ya Watanzania. Pongezi nyingi zaidi ziwaendee wale waliochaguliwa kuliwakilisha Bunge la Tanzania katika mabunge ya kimataifa.

"Mheshimiwa Rais anasema, chini ya uongozi wako Mheshimiwa Spika, Bunge la Tanzania limekuwa ni kitovu cha demokrasia Barani Afrika, jambo ambalo limesababisha kuchaguliwa kuwa makao makuu ya Sekretarieti ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola Barani Afrika.

"Halikadhalika, Mheshimiwa Rais anasema, 'Napenda kulipongeza Bunge kwa kupiga hatua kubwa kuongeza uwakilishi wa makundi ya wanawake na vijana. Huu ndio mwelekeo mzuri katika kuimarisha uwiano wa uwakilishi kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu.

"Nalitakia kila la kheri Bunge letu katika kutimiza majukumu yake. Kazi iendelee, na kwa mkono wake mwenyewe ametia sahihi hapa chini, Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania."

Kabla Spika Ndugai, hajawasomea wabunge barua hiyo ya Rais Samia alisema:

"Bunge la kwetu tunashindwa kupiga hesabu vizuri kwa sababu kuna wabunge kadhaa hawatuambii habari ya umri wao, tunashindwa...lakini kwa wale ambao wametuambia, Bunge letu liko medium (katikati) liko kwenye miaka kati ya 40, 45.

"Kwa hiyo Bunge letu, si kweli kwamba ni la vijana, wala si kwamba ni la wazee. Tuko hapo katikati, sijui tunaita nini. Umri ambao ni mzuri sana, ni wa uzoefu na ni wa kutoa maamuzi mazuri na umri wa uchapakazi. Ndio Bunge letu liko hapo.

"Duniani kote kuna wabunge kama 46,000 duniani ambao wanafanya maamuzi makubwa kwa ajili ya watu wengine."

Katika maelezo ya Spika Ndugai kuhusu maadhimisho ya Siku ya Mabunge Duniani, alisema moja ya mijadala huko mbele ya safari ni kuangalia kama Bunge moja linatosha au kuna haja ya kuwa na Bunge jingine huko juu kama nchi nyingine zilivyo.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiteta jambo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, kabla ya kufungua mafunzo kwa wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa yaliyoandaliwa na Taasisi ya Uongozi, jijini Dodoma jana, kwa lengo la kuwaimarisha kiuongozi. **PICHA: OWM**

# PM awaonya ma-RC kuendekeza kula, kuwatumia walinzi binafsi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewafunda wakuu wa mikoa na makatibu tawala kujiepusha na mambo mbalimbali yanayoweza kuathiri utendaji wao wa shughuli za umma.

Amewapa angalizo la ulaji ovyo kwenye sherehe, huku akiwataka kutotumia watu wa mitaani kama walinzi au wasaidizi wao binafsi kwa kuwa si utaratibu wa serikali.

Aidha, amesema matumizi ya sheria ya kuweka ndani watu kwa saa 48 inatakiwa kuangaliwa tena, kwa kuwa inasababisha migogoro kati yao na wananchi au wanasiasa.

Majaliwa alitoa angalizo hilo jana, alipokuwa akifungua mafunzo ya siku nne kwa viongozi hao yanayotolewa na Taasisi ya Uongozi.

Alisema wanapaswa kula nyumbani kabla ya kwenda kwenye sherehe ili wasijaze chakula kwa wingi hadi watu wawashangae.

"Umeenda kwenye sherehe Mkuu wa Mkoa ndio unaongoza watu kula, unajaza lumbesa kwenye sahani, itifaki itawaambia kabla ya kwenda kwenye sherehe uwe umeshiba nyumbani kwako ili ukienda kule unachukua kidogo tu... watasema Mkuu wa Mkoa anakula kidogo unapata heshima," alisema na kuongeza:

"Sasa wewe utoke na njaa zako ufike kwenye sherehe unakuta mabeseni yamepangwa hapa hadi kule unapita unachomoa kila aina ya chakula, naamini mtafundishwa kwenye eneo hili."

Kuhusu suala la walinzi na wasaidizi binafsi, Majaliwa alisema ofisi zao zimeandaa watu wenye taaluma husika, na si kuamua kuchukua watu wa mitaani na kuacha wale wanaolipwa mishahara kwa kazi hiyo, na kuwa huo sio utaratibu.

"Mkuu wa Mkoa unahitaji kuwa na wasaidizi, RAS ndio atakuandalia msaidizi, fursa yako wewe kama wapo wawili au watatu wewe unachagua mmoja na si kuchukua mtu mtaani, maana hana maadili ya kutunza siri za serikali, ni vizuri mkasikilizana na RAS anapokupatia msaidizi na kukupatia msaidizi ambaye utaridhika naye," alisema. "Hapa ningependa msisitizo utolewe kwa viongozi hawa kuepuka matumizi ya walinzi binafsi (bodyguards) na waandishi wa habari binafsi hadi katika ofisi za umma, kwani ndio watakuwa chanzo cha uvujaji wa siri za serikali."

Alisema serikali haitavumilia kuona miradi iliyopo katika mikoa yao inatekelezwa chini ya kiwango na kuna ubadhirifu wa fedha ndani yake.

"Katika hili, tuwe wazi na Mheshimiwa Rais amenituma niwaeleze kuwa serikali haitasita kumwajibisha kiongozi yeyote ambaye atashindwa kusimamia jambo hilo kikamilifu," alisema.

Kuhusu magari ya serikali, Majaliwa alisema isitokee hata siku moja gari la Mkuu wa Mkoa limeharibika akachukua namba ya usajili wa gari na kubandika kwenye gari lake.

"Umekwama gari mwambie RAS, kwa itifaki atatoa gari lake ili utimize majukumu yako, na atatafuta namna na si kuchukua gari yako mark II ukabandika namba za RC halafu ukatembea nayo mtaani, huku serikalini tumesema Mkuu wa Mkoa atapanda gari ya hadhi hii, na wala usije ukachukua gari lenye hadhi kubwa zaidi ya hilo ukabandika kwenye range rover kwa sababu tu Mkuu wa Mkoa anatakiwa kutembea kwenye gari la heshima," alisema.

Aliongeza kuwa suala jingine la itifaki ni kusikiliza simu za viongozi wa juu na si kuzipuuza.

"Waziri Mkuu anapiga simu unaiona halafu unasema mimi nina shughuli zangu unaweka pembeni, sio itifaki, kiongozi wa juu anapokupigia ana jambo unatakiwa kutoka pembeni hata kama upo kwenye mkutano kumsikiliza na baadaye kuendelea na shughuli zako," alisema.

Aliwataka kutambua ofisi na majukumu yao ili kusiwe na migogoro kati yao na viongozi wenzao au mihimili mingine.

"Wewe Mkuu wa Mkoa, kiongozi wa shughuli zote kwenye mkoa kuna mhimili kuna Hakimu, Jaji, ofisi kwako kuna Katibu Tawala wote mmeteuliwa na Rais, lazima kusiwapo na kutunishiana misuli kwa kuwa kila mmoja, kuna watu walikuwa wanakwaruzana maofisini. Kuna mahali aliendа Mkuu wa Mkoa kwenye wilaya Mkuu wa Wilaya anasema sina taarifa zako nina ratiba zangu."

"Kuna migogoro mingi kati ya Wakuu wa Mikoa na Mawaziri, Mawaziri pia watakuja hapa ili nao tuwe na mfumo wa kusomana vizuri, nimewahi kushuhudia kusini kule, waziri ameenda kukaa kwenye kiti cha Mkuu wa Mkoa, anakuja Mkuu wa Mkoa anamkuta Waziri amekaa anamwambia mimi ndio Mkuu wa Mkoa ondoka, mbele za watu wasaidizi wamejipanga mapema wanashuhudia viongozi wanagombea viti."

"Kuna Mkuu wa Wilaya alitembelewa na DC mwenzake anasema mbona umekuja bila taarifa mimi nina ratiba zangu, mara akamuita OCD watu wakasema hapana hapana, basi akaondoka zake... mkuu wa wilaya mgeni, jamani akija mwenzako mpokee vizuri."

Kuhusu viongozi waliostaafu, Majaliwa alisema viongozi hao lazima waheshimiwe, kwa kuwa wanastahili kupewa heshima hata kama wamestaafu.

Akizungumzia suala la utunzaji wa siri, Majaliwa aliwataka viongozi hao kuhakikisha wanasimamia na kudhibiti utunzaji wa siri za serikali kutokana na kuibuka kwa wimbi la baadhi ya barua kukutwa kwenye mitandao ya kijamii.

"Ni aibu Mkuu wa Mkoa barua ya Mkoa wako kuonekana Whatsapp, huo sio usiri wa nyaraka za serikali... hii tabia imeibuka sana hivi karibuni kutokana na kuibuka kwa mitandao yetu, siri ndio uhai wa serikali yetu, mnatakiwa kusikiliza kwa umakini mkubwa,"alisema.

Awali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu, alisema atawasilisha mapendekezo ya kuwapima viongozi hao na Wakurugenzi wa Halmashauri wote nchini kwa kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya wananchi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohammed Mchengerwa, alisema anaamini mafunzo hayo yatawafanya kuwa viongozi bora na sio watawala katika maeneo yao.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi, Kadali Singo, alisema mafunzo hayo ni utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Waziri Mchengerwa ya kuhakikisha taasisi hiyo inafikia viongozi katika wizara, idara na taasisi zote.

Alisema tangu kuanzishwa kwake mwaka 2010 wamewafikia wakuu wa mikoa, wilaya, makatibu tawala wa mikoa na wilaya, pamoja na wakurugenzi 7,000 huku akitaja mada 10 zitakazofundishwa kwa viongozi hao kuwa ni masuala ya itifaki, maadili ya uongozi na rushwa na usuluhishi wa migogoro ili kuimarisha uwezo wao kwenye utekelezaji wa majukumu.

## CUF 'yamlilia' Rais Samia Katiba Mpya

**Na Enock Charles**

MWENYEKITI wa Chama cha Wananchi (CUF), Profesa Ibrahim Lipumba, amemwomba Rais Samia Suluhu kulipa kipaumbele suala la Katiba Mpya, akiamini itasaidia kulinda uchumi atakaoujenga katika kipindi chake cha uongozi.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye Makao Makuu ya chama hicho jijini Dar es Salaam jana, Profesa Lipumba alisema kuwa amesikitishwa na kauli ya Rais Samia aliyoitoa juzi wakati wa mkutano na wahariri wa vyombo vya habari kuwa suala la Katiba Mpya lisubiri ajenge uchumi kwanza.

Profesa Lipumba alisema CUF wanaamini Katiba na uchumi ni vitu vinavyotakiwa kwenda pamoja.

"Tumekuwa tukiambiwa kwamba tumefikia uchumi wa kati sasa. Je, anataka tufikie uchumi wa juu ndiyo tushughulikie suala la Katiba?" Profesa Lipumba alihoji.

"Rais aliahidi kukutana na vyama vya siasa kuzungumzia demokrasia nchini lakini bado hajatimiza mpaka sasa," aliongeza.

Profesa Lipumba alimshauri Rais Samia kujiwekea malengo binafsi ya kuchukua tuzo ya Mo Ibrahimu ambayo hutolewa kwa viongozi walioongoza vizuri hasa katika suala la demokrasia, kupambana na ufisadi na kupunguza umaskini kwa wananchi wao na kutokusubiri mpaka wananchi waandamane kudai Katiba.

Alisema demokrasia ni nyenzo bora ya kujenga uchumi shirikishi na Katiba ni hitaji la msingi kwa wananchi kuliko kuwa maslahi binafsi kwa wanasiasa, hivyo akamwomba Rais kumalizia mchakato huo ulioanza katika kipindi cha serikali ya awamu ya nne huku yeye mwenyewe (Rais Samia) akiwa Mwenyekiti Mwenza wa Bunge Maalum la Katiba.

Kuhusu mikutano ya vyama vya siasa, Profesa Lipumba alisema hata Katiba iliyopo sasa haimpi mamlaka Rais kuizuia na kwamba kufanya hivyo ni kinyume cha matakwa ya sheria na kumsihi Rais Samia kutimiza ahadi yake ya kukutana na viongozi wa vyama vya siasa.

Vyama kadhaa vya upinzani, vikiwamo ACT-Wazalendo na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) tayari vimeshatoa matamko ya kusikitishwa na kauli ya Rais Samia kuhusu msimamo wake dhidi ya mchakato wa Katiba Mpya na mikutano ya kisiasa nchini.

# Muswada wabainisha ajira 15,000 katika bomba mafuta

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SERIKALI imetangaza neema ya ajira mpya kwa Watanzania 15,000 watakaoshiriki mradi mkubwa wa uwekezaji wa bomba la mafuta ghafi linalojengwa kutoka Hoima nchini Uganda hadi Bandari ya Tanga.

Jana, Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alitangaza neema hiyo wakati akichangia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Namba 3 wa Mwaka 2021, ulioingizwa Bungeni kwa hati ya dharura na kujadiliwa na wabunge.

Mradi huo wenye urefu wa kilomita 1,145, unajulikana kama East African Crude Oil Pipeline (EACOP).

"Nafasi zote hizi ni za Watanzania, zaidi ya asilimia 80 ya ajira zitatoka Tanzania. Wafanyakazi wapatao 15,000 wakati wa ujenzi wa mradi huu wataajiriwa.

"Nitoe wito kwa Watanzania wenye uwezo waende kuchangamkia fursa hizi, iwe mamantilie, iwe kampuni za ulinzi, kampuni za usambazaji, zote zitafanywa na Watanzania. Tunaweka msisitizo zaidi kwamba vifaa vyote vya bomba iwe saruji, nondo, misumari ni lazima vitokane na viwanda vyetu vya ndani."

Kwa mujibu wa Waziri Kalemani, Watanzania hao watanufaika na ajira za moja kwa moja kwenye makambi 12 yaliyopo Tanzania kati ya 14 yaliyojengwa katika mradi huo. "Manufaa ya mradi huu ni makubwa sana kwa hizo takribani kilomita 1,145 zinazojengwa ziko Tanzania. Tutakuwa na vituo vya kupasha joto bomba la mafuta 29 na vituo 22 viko Tanzania.

"Mahali pa kufungulia valve (mifuniko) viko vituo 76, vituo 53 viko Tanzania, lakini kuna vituo sita (6) vingine vya kusukuma na kupunguza mgandamizo wa mwendo kasi wa mafuta, vinne viko Tanzania na kutajengwa matangi matano makubwa Chongoleani."

**WARATIBU MRADI**

Aidha, Kalemani alisema kwa kuwa mradi huo ni wa kimkakati na usimamizi wake ni lazima uwe ni wa kimkakati, wizara hiyo imeunda timu mahususi na imeshateua waratibu wa mradi huo ambao ni Watanzania vijana waliobobea kwenye masuala ya mafuta.

Timu tayari imekabidhiwa jukumu la kuanza kazi, baada ya kuteuliwa miezi miwili iliyopita.

"Sehemu ya pili ya usimamizi, tumeunda chombo kinaitwa Government Facilitation Team (Timu ya Uwezeshaji ya Serikali), badala ya kusubiri vibali mahali ambapo watahitaji vibali vya wataalamu kuhusu utekelezaji wa mradi, tumeweka mamlaka kwa kuteua wataalamu waandamizi ili kusaidia katika uratibu wa mradi.

"Mathalani labda kibali kinahitajika kutoa exception TRA (msamaha wa kodi kutoka Mamlaka ya Mapato), tumemtaka na kumuomba Kamishna Mkuu wa TRA kuteua Ofisa ambaye atakuwa Desk Officer (Ofisa Maalum) ili jambo likifika lisilale wala kuchelewa; na tumefanya hivyo katika sekta zote za serikali.

"Hii inasaidia sana kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa mradi huu ili kuendana na wakati kwa manufaa ya Watanzania. Jambo la pili kimuundo, asilimia 80 ya mradi huu uko kwetu. Niwaombe mahali ambapo bomba litapita, sisi tuwe watu wa kwanza kulinda bomba na ni sehemu ya usimamizi.

"Tumepitisha utaratibu ambao utatumika katika kila kata, tarafa na wakuu wa wilaya watakuwa wasimamizi wa kwanza kuhakikisha vijana wenye uwezo wa kufanya kazi hizi, ndio wanapata ajira wa kwanza."

Vile vile, alilieleza Bunge kuwa wameanzisha kanzi data ambayo inasajili makampuni ya ndani ambayo yatafanya kazi zote za usambazaji, ujenzi, za kutoa huduma wamesajiliwa EWURA. Kampuni zote zitakazotoa huduma zote ni za ndani. "Tuwaambie makandarasi wenye uwezo waende kujisajili EWURA ili waweze kupata fursa ya kufanya kazi hizi wakati wa utekelezaji wa mradi huu."

**SEKTA BINAFSI KIPAUMBELE**

Kalemani alisema serikali inakusudia kukutana na sekta binafsi kupata maoni na mapendekezo yao ya namna ya kuvutia vijana kuajiriwa katika mradi huo mkubwa.

"Tutafanya semina na 'Private Sector Foundation', ile taasisi tunakaa nayo itupe mkakati na yenyewe ya namna ya kuchukua fursa hii. Tunafanya mkutano mkubwa kule Chongoleani, Tanga Julai 3, mwaka huu.



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Sayansi na Teknolojia nchini (COSTECH), Dk. Amos Nungu, akizungumza na wabunifu mbalimbali 25 wakati wa kubadilishana uzoefu ili kuwasaidia vijana maarifa ya kujikwamua kiuchumi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Vitambulisho vya machinga vyaingiza serikalini bil. 46.71/-

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema tangu kuanza kwa utoaji wa vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo maarufu 'machinga,' serikali imekusanya zaidi ya Sh. bilioni 46.71 Tangu kuanza kwa zoezi hilo la kuwatambua wafanyabiashara na watoa huduma wadogo nchini, kwa kuwapatia vitambulisho na kuwawekea mazingira rafiki ya kufanya biashara, machinga waliofikiwa ni 2,335,711 vimegawiwa.

Wakati anasoma hotuba yake ya kuliahirisha Bunge jana, Majaliwa, alisema: "Katika mwaka wa fedha 2020/2021, serikali iliamua kuboresha vitambulisho hivyo kwa kuweka picha na jina la mjasiriamali ili kuongeza udhibiti.

"Ni kuwawezesha wajasiriamali kutumia vitambulisho hivyo kupata huduma za kibenki na bima ya afya. Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na TRA itaendelea na utaratibu wa kusajili wajasiriamali hao kwa kutumia mfumo, kuchapisha vitambulisho na kuvisambaza kwa halmashauri husika ili vigawiwe."

Vitambulisho vya machinga vilibuniwa na kugawiwa kwa mara ya kwanza kwa wajasiariamali 675,000 na Hayati Rais Dk. John Magufuli mwaka 2018, kwa ajili ya kuwatambua wafanyabiashara wadogo nchini kuhakikisha wanafanya shughuli zao bila kusumbuliwa.

Aidha, Waziri Mkuu Majaliwa, alisisitiza kuwa serikali ya Rais Samia itayatilia mkazo maeneo ya kuvutia uwekezaji, upatikanaji wa ujuzi, sensa ya watu na makazi na vitambulisho vya wamachinga.

Maeneo mengine ni udhibiti wa magonjwa ya mlipuko, upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, Bima ya Afya kwa Wote, kuimarisha kilimo na hifadhi ya mazingira. Alisema, serikali iko katika hatua za mwisho za kukamilisha utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi nchini, ambao utatoa taswira ya hali halisi ya ujuzi, ikijumuisha viwango vya ujuzi wa chini, wa kati na wa juu katika nchi yetu.

# Mfugale kuagwa leo Dodoma, Samia amlilia

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemlilia Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandisi Patrick Mfugale, aliyefariki dunia juzi jijini Dodoma baada ya kuugua ghafla.

Mhandisi Mfugale anatarajia kuagwa leo jijini Dodoma katika Hospitali ya Benjamin Mkapa na anatarajia kuzikwa Jumatatu Ifunda, mkoani Iringa.

Katika salamu zake za rambirambi, Rais Samia kupitia ukurasa wake wa Twitter aliandika: "Nimesikitishwa na taarifa ya kifo cha Mhandisi Patrick Mfugale (Mtendaji Mkuu, TANROADS). "Nitaukumbuka mchango mkubwa katika ujenzi wa miundombinu yetu hasa barabara, madaraja, reli na umeme. Pole kwa familia na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mungu amweke mahali pema peponi, Amina."

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa katika ukurasa wake wa Instagram aliandika: "Lala salama Mhandisi Patrick Mfugale nitakukumbuka daima kila nitakapoona kazi za uhandisi na uongozi wako; Flyover ya Mfugale pale TAZARA, Dar es Salaam itanikumbusha mara nyingi zaidi, daraja la JPM (Kigongo), Busisi litanikumbusha kila nitakapopita Kanda ya Ziwa.

"Kijazi Interchange (Ubungo), daraja la Tanzanite (Aga Khan, Coco Beach), barabara za mwendokasi, reli (SGR) vitanikumbusha mara zote nikiwa Dar es Salaam, bwawa la Nyerere kule Rufiji, Megawati 2,115 zitanikumbusha, barabara za lami na madaraja nchi nzima yatanikumbusha daima, TANROADS ambayo umekuwa Mtendaji Mkuu kwa miaka 12, umemaliza kazi, utavalishwa taji."

**RATIBA YA MAZISHI**

Ratiba ya mazishi inaonyesha baada ya kuagwa Dodoma mwili huo utasafirishwa kwenda mkoani Dar es Salaam na kuhifadhiwa Hospitali ya Lugalo na utaagwa siku inayofuata (Julai 3) na jioni kusafirishwa kuelekea Ifunda, Iringa.

Jumatatu shughuli ya maziko itafanyika nyumbani kwao Ifunda, baada ya ibada na heshima ya mwisho kufanyika.



Mkurugenzi wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi (katikati), akifungua kongamano kuzungumzia siku 100 za Rais Samia Suluhu Hassan, katika viwanja vya mtandao huo, Mabibo, mkoani Dar es Salaam jana, Kulia ni Mwakilishi wa Ongawa, Dario Garcia na Mwanaharakati Dina Mbaga. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA**

# Magereza yaja na mkakati kupunguza msongamano

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Magereza limesema linaanza utekelezaji mkakati wa ujenzi wa magereza mapya katika wilaya 46 nchini, ili kuondokana na uhaba, jambo linalosababisha wafungwa kubanana.

Aidha, wamepata maeneo katika wilaya 26 kwa ajili ya ujenzi wa magereza, na kwamba bajeti ya utekelezaji iko tayari.

Kamishna wa Jeshi hilo, Seleman Mzee, aliyasema hayo katika mahojiano maalum na Nipashe jijini Dodoma, kuhusu namna wamejipanga kuongeza magereza kutokana na ukweli kuwa idadi ya watu inaongezeka.

Pia, jeshi hilo limesema litaendelea kujenga ngome kwenye magereza ambayo hayana ili kupokea wafungwa na mahabusu wa aina yoyote. "Tunakabiliwa na uhaba wa magereza kutokana na idadi ya mahabusu na wafungwa inavyoongezeka, hali hii itaendelea kuwa mbaya hasa ukizingatia ongezeko la watu nchini. Moja ya mikakati ni kujenga magereza mapya katika wilaya zote ambazo hazina magereza," alibainisha.

Kwa mujibu wa Mzee, ngome zilizojengwa ni Mkono wa Mara ilioko Morogoro, Gereza Rombo, Kilimanjaro, Gereza Kihondo ambayo inaanza kujengwa na Ngome ya Gereza Ileje, mkoani Songwe imeshakamilika.

Alizitaka mamkala za Polisi na Mahakama ambazo zinahusika na mahabusu kuchukua hatua stahili kwa kutimiza wajibu wao hasa katika uendeshaji wa kesi ili kupunguza idadi ya mahabusu kwenye magereza.

Kamishna huyo alisema jeshi hilo linaendelea kupunguza wafungwa kupitia taratibu za kisheria kupitia misamaha kwa wanaostahili.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maazimio ya mawaziri 8 yatekelezwe kwa vitendo

**JUZI** mawaziri wanane waliweka bayana mkakati wa pamoja katika kukabiliana na kelele nyumba za ibada na maeneo ya starehe, huku wakiweka adhabu kali, ikiwamo kufunga biashara au eneo husika ambalo ni kero kwa waliolalamika.

Adhabu iliyopo kwenye Sheria ya Mazingira ni kifungo cha miezi sita jela na kufungiwa biashara kwa watu watakaobainika kusababisha kelele na mitetemo kwenye makazi ya watu hasa kwenye nyumba za ibada na starehe. Mawaziri hao ni kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira); Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI); Ofisi ya Waziri Mkuu (UWEKEZAJI); Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Wizara ya Viwanda na Biashara; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Waziri wa Mazingira, Selemani Jafo, alieleza mikakati mitano yenye lengo la kuondokana na hali hiyo, ikiwamo kutilia mkazo utekelezaji wa Kanuni za Usimamizi wa Mazingira za mwaka 2015.

Pia wamewataka wenye nyumba za ibada na maeneo ya starehe kuhakikisha shughuli zake hazisababishi kelele na mitetemo na sauti ziwe kwa kiwango kinachokubaliwa kisheria.

Hii ni habari njema sana kwa wananchi wengi wa maeneo ya mjini, ambao wameishi kwa mateso na usumbufu kwa muda mrefu, huku baadhi ya mamlaka zikitumia kama sehemu ya kujipatia fedha kwa kupokea rushwa hasa kwa wamiliki wa maeneo ya starehe.

Licha ya sheria kutaka kuwa inapofika saa sita usiku maeneo ya starehe kushusha sauti, lakini inakuwa kinyume kwa kuwa badala yake huzidisha. Eneo gumu sana ambalo limekuwa kero, lakini viongozi wanaogopa kuligusa ni nyumba za ibada ambazo zinaanzishwa kila uchao kwenye makazi ya watu, na mara nyingi wanakuwa na mitetemo mikubwa kiasi cha kulazimu waliopo jirani kutolala usiku kucha. Kwa sasa watu wanabadili makazi yao na kuanzisha makanisa kwa ajili ya kumwabudu Mungu. Ni jambo jema, lakini katika ibada hizo isiwe kero kwa wengine, ni lazima kusheshimu wengine kwa kuwa hata Mungu ameagiza binadamu kuheshimu wengine na kuishi kwa upendo. Ni muhimu mkakati huu wa mawaziri wanane ukawa kwa vitendo na ufuatiliaji usiwe wa kueleza umma tu na kumaliza, kwa kuwa hakuna ubishi kelele ni kero kubwa sana hasa nyakati za usiku katika maeneo ya watu. Kutoa taarifa halafu mamlaka kukaa kimya, ni jambo linaloonyesha kuna rushwa.

Mathalani, wakazi wa Banana Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam wanaishi kwa taabu kwa kuwa kuna baa tatu sugu na nyumba za ibada kwa kupiga muziki na ibada hadi asubuhi, na mbaya zaidi mamlaka za serikali zinajua, lakini hatua hazichukuliwi. Hawa ni mfano kati ya wengi.

Ni muhimu hatua mahususi zikachukuliwa kwamba mtu kabla hajapewa kibali cha kuanzisha nyumba ya ibada au eneo la starehe, awe amekidhi vigezo vyote na afuatiliwe kwa karibu kwa kutumia mamlaka za serikali za mitaa na Polisi, kuhakikisha anafuata masharti ya leseni au kibali chake. Ikiwa hali itaachwa hivi, kuna hatari kubwa ya kujikuta uchumi unatikiswa na watu kushindwa kufanyakazi, mzigo wa matibabu kwa watu ambao hawapumziki.

Hata kama watu hawa wana haki ya kikatiba ya kuabudu, lakini ni vizuri wafanye hayo bila kuwa kero kwa wengine, hata kama nchi inataka kodi kutokana na biashara, lakini wasikwaze walipakodi wengine. Tunapaswa kujifunza kwa nchi zilizoendelea, ambazo huwezi kukuta baa na nyumba za ibada ni kero kwa watu, kwa kuwa zimejengwa kwa muundo wa kuhakikisha sauti inabaki ndani kwa ndani.

Ikiwa mamlaka za serikali zitashirikiana kikamilifu maana yake kero hii itaondoka, lakini Wizara ya Mambo ya Ndani inapaswa kufuatilia kwa karibu. Pia Wizara ya Ardhi wanaotoa vibali vya kubadili matumizi ya eneo husika ni muhimu kufuatilia kwa kina kabla ya kufanya uamuzi. Hata Mungu alisema asiyefanyakazi asile na anataka watu wafanyekazi ili wapate fedha walipe kodi. Na ndiyo maana kwenye Biblia inaelezwa kuwa ya Kaisari mpe Kaisari na ya Mungu mpe Mungu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Matrafiki niwadokeze, abiria wanakalishwa kwenye ndoo



Na Yasmine Protace

**NAJUA** kuna mitandao mtambuka katika mifumo ya usafiri barabarani. Lakini, walau kuna eneo moja la kutajwa ambao ndio wenyeji Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, wakiwa wasimamizi wakuu wa sheria na maagizo yanayotolewa.

Kuna kila sababu ya kuanza kuipongeza timu nzima ya usimamizi, kwa maana ya wanaowajibika na eneo hilo kama vile Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA). Ipo wazi kuna kazi kubwa inafanyika tena kwa jasho jingi kufanikisha mahitaji stahiki, hata ambao yakaenda sawa.

Pamoja na pongezi hizo, pia niweke sawa kuwapo magumu yanayoshuhudiwa nchini, kwa mabasi yanayosafiri kati ya mkoa mmoja na mwingine, ingawaje kwa sehemu kubwa ni safari inayoungana na ama mwanzo au kuishia jijini Dar es Salaam.

Katika safari hizo zinazoendelea, huwa kuna tabia ya baadhi ya mabasi kuweka ndoo, ili abiria wazikalie, wakipewa tiketi ya basi tiketi isiyo na tarehe wala jina la kampuni inayomiliki basi hilo.

Huwa naangukia mshangao kwamba tiketi zinatolewa na hazina namba za simu zinazotakiwa kuwekwa kisheria zenye maana kubwa, ikiwamo panapotokea tatizo abiria anaweza kuipiga namba hiyo kuhoji au kutaarifu mamlaka inayohitajika kwa wakati huo.

> **Huwa naangukia mshangao kwamba tiketi zinatolewa na hazina namba za simu zinazotakiwa kuwekwa kisheria zenye maana kubwa, ikiwamo panapotokea tatizo abiria anaweza kuipiga namba hiyo kuhoji au kutaarifu mamlaka inayohitajika kwa wakati huo.**

Sote tunajua kazi ya ndoo ni ipi; inahifadhi taka, lakini kutokana na kupakiwa, abiria hulazimika kutupa taka nje ya madirisha.

Pia, abiria anapopewa tiketi yenye vigezo inamsaidia hata akipata ajali ni rahisi kulipwa haki yako. Iwapo namba za tiketi hazikupewa jina la kampuni, nayo inachangia kumwathiri abiria mhitaji kwa wakati huo.

Nina rai kwa askari Polisi mliopo maeneo ya stendi au barabarani na kwingineko kwenye usafiri wa barabara kuu wa mabasi na magari mengine, daima mnatakiwa kuwa makini pale mnapozisimamisha kwenye njia kuu, muwe mnaingia ndani ya magari kusikiliza taarifa kutoka kwa abiria.

Uzoefu wangu wa safari hizo, wapo polisi wanaoingia ndani ya magari kukagua na wapo wasioingia katika magari, wanabaki nje wakiwahoji madereva.

Iwapo wakiingia ndani ya mabasi, ninaamni wataona mengi sana yalioyofichwa na ukiukwaji uliopitiliza wa sheria zilizopo za usalama wa umma na vyombo vyake.

Utakuta abiria analipa nauli, lakini amekalishwa kwenye ndoo, pia basi linakuwa na mikanda haieleweki na kwa jumla ni hali mbaya. Abiria hajui wa kumwambia amfunge mkanda.

Pia, kuna ukatishaji tiketi usioeleweka na baadhi ya mabasi yanatumia wakala wake wanaowarubuni abiria, kwa kuwadanganya gari itaishia stendi fulani na mwisho wa siku gari haifiki iliko stendi walioahidi.

Abiria anapochukua hatua ya kulalamika, anajibiwa ya mkato kuwa wakala walikata tiketi tu na awakusafiri, hivyo hawahusiki na malalamiko hayo.

Sasa inaacha maswali yenye vitendawili, abiria huyo anaipata wapi haki yake? Hatua ya mwanzo ya utatuzi ni kwa polisi barabarani, waingie ndani kujionea mambo yanavyoendelea katika mabasi hayo.

HABARI KITAIFA

# WMA yataka watumiaji wa gesi kuhakiki mitungi

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Vipimo (WMA), umewataka wananchi kuhakikisha wana hakiki mitungi ya gesi kama ina ujazo sahihi ulioandikwa kabla ya kuondoka nayo wanapoinunua kutokana na baadhi ya wauzaji kupunguza ujazo.

Hayo yalisemwa jana na Meneja wa WMA Mkoa wa Kagera, Harrieti Lukindo, wakati akizungumza kwenye viwanja vya maonyesho ya kimataifa vya Mwalimu Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Alisema Watanzania wengi wamekuwa wakipunjwa kwenye mitungi ya gesi kwasababu hawana mwamko wa kuhakiki mitungi hiyo wanapoenda kununua madukani.

"Kwanza Watanzania wengi hawaendi wenyewe wanawatuma watu wa bodaboda ndiyo maana wanachukua bila kuipima, lakini unapaswa kuuhakiki mtungi wako kwenye mzani ambao kila muuzaji wa gesi anatakiwa kuwa nao kwa mujibu wa sheria," alisema.

Alisema WMA imekuwa ikifanya ukaguzi wa kushtukiza na mara kadhaa wanakuta baadhi ya mitungi ikiwa na upungufu wa ujazo uliaondikwa kwenye mtungi husika hivyo kumpunja mlaji.

"Lazima mnunuzi ajiridhishe kwamba mtungi wake haujachezewa ahakikishe alama ya kufungia (seal) kwenye mtungi husika haijafunguliwa kwasababu baadhi huwa wanapunguza kilo na kuhamishia kwingine," alisema.

Naye Ofisa Vipimo wa WMA, Mkoa wa Ilala, Glory Mtana, aliwataka Watanzania wenye wasiwasi na mita zao za maji kutoa taarifa kwa mamlaka hiyo ili ziweze kuhakikiwa kama zina ubora unaokubalika kisheria.

Alisema miongoni mwa mambo wanayofanya kwenye maonyesho hayo ni kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuhakiki mita za maji ili wapate bili sahihi kutoka kwa mamlaka.

Alisema WMA imekuwa ikihakiki mita za maji ili kuhakikisha Watanzania wanalipia kiasi sahihi wanachotumia na mamlaka husika kupata malipo yanayostahili.

"Ili kujua kwamba hii mita imehakikiwa lazima iwe na alama ya kufungia (seal) ya serikali watu wanaofungiwa mita za maji wazingatie hili ili wapate huduma sahihi," alisema.

Alisema mbali na mita za maji, WMA tayari ilishaanza kuhakiki mita za umeme ili kuhakikisha watumiaji wa nishati hiyo wanalipia kiasi tu walichotumia na si vinginevyo.

Alisema mita hizo za maji na umeme zimekuwa zikihakikiwa kwenye kituo cha Misugusugu Mkoa wa Pwani kabla ya kwenda kwa watumiaji ili kuepusha malalamiko kwa wananchi kuletewa bili isiyo sahihi.

Alisema pia wamekuwa wakihakiki mizani inayopima madini, kuhakiki vipimo katika sekta ya kilimo na kuhakiki bidhaa zilizofungashwa.




Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Kagera, Harrieti Lukindo, akiwaelezea wananchi waliofika kwenye banda hilo kuhusu uhakiki wa mitungi ya gesi kwenye Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa yanayoendelea katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wenyeviti Mitaa watishia kugoma

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WENYEVITI wa serikali za mitaa, vitongoji na vijiji katika Manispaa ya Shinyanga wametishia kususa kufanya kazi na Mkurugenzi wa Manispaa hiyo na kutoshiriki vikao vya maendeleo ya kata kwa kile wanachodai kutothaminiwa na kutokulipwa posho zao za kila mwezi.

Viongozi hao walibainisha hayo juzi kwenye kikao chao cha dharura cha wenyeviti wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji.

Wenyeviti hao wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye kikao hicho walisema posho zao ambazo ni Sh. 15,000 kila mwezi, hawalipwi kwa wakati na wakiwasilisha malalamiko yao kwa mkurugenzi, hayafanyiwi kazi.

Mmoja wa wenyeviti hao, Majid Issa kutoka Mtaa wa Majengo Manispaa ya Shinyanga, alisema maazimio ya wenyeviti hao wa serikali za mitaa ni kususia kufanya kazi na mkurugenzi na kutoshiriki kwenye shughuli zozote za maendeleo hadi pale kilio chao kitakaposikilizwa.

"Kuanzia sasa hatutashiriki kwenye shughuli zozote zile za maendeleo ya kata, wala kufanya kazi na mkurugenzi hadi tulipwe posho zetu pamoja na shughuli za uzoaji wa taka ngumu zirudishwe kwenye serikali za mitaa ili tupate fedha za kuendesha ofisi zetu ikiwamo kulipia ofisi na vitendea kazi," alisema Issa.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mwamala, Juma Maswa, alidai wenyeviti hao wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu.

Alisema baadhi yao hawana ofisi wala vitambulisho vinavyowatambulisha kuwa wao ni wenyeviti wa serikali za mitaa.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Doris Dalio, alisema malalamiko ya wenyeviti hao yanafanyiwa kazi, likiwamo suala la kuwalipa posho wanazodai za miezi miwili, huku akikiri kuwapo na upungufu wa ofisi na mkakati unaoendelea kufanyiwa kazi ni kuwajengea ofisi kulingana na hali ya ukusanyanji wa fedha za mapato ya ndani.

# Bil. 4.6/- zatumika miradi ya maendeleo

**Na Steven William,** IRINGA

ZAIDI ya Sh. bilioni 4.6 zimetumika kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo wilayani Iringa, ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa ilani hiyo juzi katika kikao cha Halmashauri Kuu ya Wilaya ya Iringa Mjini kwenye Ukumbi wa Siasa ni Kilimo, Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, alisema miradi hiyo imegharimu Sh. 4,642,758,198.07.

Kwa mujibu wa Moyo, kiasi hicho cha fedha kimetumika katika kipindi cha Januari hadi Juni, mwaka huu.

Moyo alitaja miradi hiyo kuwa ni katika sekta ya elimu (msingi na sekondari), kilimo, afya, mifugo na uvuvi, viwanda na biashara, utawala bora na maendeleo ya jamii.

Mkuu huyo wa wilaya aliwapongeza viongozi wa ngazi mbalimbali kwa usimamizi wa miradi hiyo pamoja na fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji huo. Hata hivyo, mkuu huyo aliwaonya viongozi wa ngazi za vitongoji, vijiji na kata wa CCM kwa tabia yao ya kujifanya miungu watu kwa kunyanyasa wananchi katika maeneo yao na kuwataka waache mara moja. Alisema kuwa kumekuwa na tabia ya baadhi ya viongozi wa CCM katika kata kujifanya wako juu ya sheria na kuanzisha migogoro ndani ya chama na wananchi.

Moyo alisema lazima viongozi wa CCM kuanzia ngazi ya shina mpaka kata wajenge umoja, upendo na mshikamono kwa viongozi wenzao na wananchi badala ya kujiona ni wakubwa na kutumia nafasi zao kinyume cha sheria. Aliwaambia viongozi hao kwamba hivi sasa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 umemalizika, hivyo kinachotakiwa ni kuchapa kazi na kuondoa makundi ndani ya chama.

"Bado kuna watu wanaendekeza makundi ndani ya CCM eti kwa sababu watu wao waliokuwa wanawataka wameshindwa. Huu si muda wa kufanya hivyo, acheni makundi na kuungana kutekeleza ilani ya uchaguzi ambayo ilitumika kujinadi kwa wananchi na hatimaye kukipatia chama kura," alisema.

Wakati huo huo, Moyo amewataka viongozi wa kisiasa na wa serikali kwenye ngazi zote kutoa elimu kwa wananchi juu ya kujikinga na corona pamoja na Ukimwi.

# Bil. 2.3/- kutoa vifaa, elimu ya Covid-19 kwenye baa

**Na Christina Mwakangale**

SHILINGI bilioni 2.3 zinatarajiwa kutumika katika mpango maalumu wa kutoa elimu, kusambaza vifaa ikiwamo vitakasa mikono na sabuni, kupambana na ugonjwa wa Covid-19 kwenye mikoa mitatu pamoja na Zanzibar.

Mpango huo uliopewa jina la 'Tunyanyuke Pamoja' utazifikia baa zaidi ya 2,000 mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia Julai mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Serengeti Breweries Limited (SBL), Tanzania, Mark Ocitti, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa mikoa hiyo imechaguliwa kuanza kupata huduma hiyo kabla ya mikoa mingine, kutokana kuwa na idadi kubwa zaidi ya kupokea wageni ikilinganishwa na mingine.

Ocitti alikuwa akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu mpango huo, na kwamba watoa huduma kwenye baa wanaweza kufikiwa kwa kutuma maombi kupitia mtandao tovuti ya www.diageobaracademy.com.

"Corona imebadili mfumo wa maisha ya kijamii ambao ulizoeleka na kuathiri huduma zinazotolewa katika biashara tofauti ikiwamo baa na maeneo ya utalii, ambako watu hukusanyika kwa ajili ya kupumzika, kuburudika baada ya kazi," alisema Ocitti.

"Lengo ni kunyanyua tena shughuli za wenye baa na kuunga mkono juhudi za serikali kupambana na corona kwa kuelimisha wahudumu, wamiliki na wateja wanaofika baa. Kuzingatia umbali baina ya mtu na mtu, kutumia vitakasa mikono na kunawa mikono."

Alisema mpango huo ni kwa ushirikiano kati ya SBL na Crisis Revolving Centre (CRC), ambao kwa pamoja watahamasisha wafanyabiashara na wateja kuweka mazingira safi ya kujikinga na magonjwa ya kuambukiza ikiwamo Covid-19.

Mkurugenzi wa Mahusiano kwa Umma SBL. John Wanyancha, alisema kampuni hiyo imeanza kupokea maombi kwa kuhamasisha watoa huduma kwenye baa kutumia fursa hiyo ili kuinua biashara.

Mmoja wa wasambazaji wa vinywaji, Kelvin Tegwa, alisema elimu katika baa ni muhimu kwa kuwa ni kati ya meneo ambayo wananchi hufika kwa wingi kwa ajili ya kujipumzisha.

Fredrick Mramba, Mkurugenzi wa Nyumrina Mramba Park, alisema corona tangu iingie nchini athari kwenye biashara zao za vinywaji ni pamoja na kuporomoka kwa idadi ya wateja kutokana na awali walihudumia 100 hadi 150, lakini idadi imeshuka hadi wateja watano kwa siku..

# Kampuni yapata cheti ubora kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Davis & Shirtliff Tanzania, imekabidhiwa cheti cha ubora kutoka Shirika la Kimataifa la Usimamizi wa Viwango (ISO), hatua ambayo ni kubwa kwa kampuni ya Kitanzania kutokana na kuboresha maisha ya watu kupitia huduma za maji.

Cheti cha ISO 9001 ni uthibitisho kwamba kampuni imekidhi vigezo vya usimamizi wa ubora kwa mujibu wa mfumo wa usimamizi unaokubalika kimataifa.

Akizungumza wakati wa kukabidhi cheti hicho, Mkurugenzi Mtendaji wa Davis & Shirtliff Tanzania, Benjamin Munyao, alisema: "Moja ya misingi yetu ni ubora. Kwa hiyo cheti hiki ni msisitizo wa ubora wa wafanyakazi wetu, vifaa vyetu na utendaji kazi kwamba uko katika viwango vya juu sana."

Kupitia hatua hiyo, alisema kampuni inaweza kufanya kazi kitaifa na kimataifa kwa kuwa mashirika mengi yanahitaji kufanya kazi na kampuni ambazo zimethibitishwa na ISO.

"Kwa zaidi ya miaka 20 tumekuwa tukiendesha biashara hapa Tanzania kwa kuhakikisha tunatumia rasilimali watu, teknolojia na rasilimali mbalimbali kuboresha maisha ya watu kupitia kutoa suluhisho mbalimbali za kudumu kwenye sekta ya maji," alisema.

Aliongeza kuwa lengo la muda mrefu ni kuhakikisha wanaleta matokeo chanya kwa jamii ili kuhakikisha rasilimali maji inatumika kwa ufanisi ili kudumu kwa vizazi vijavyo.

Davis and Shirtliff ni kampuni inayoaminika katika utengenezaji na usambazaji wa bidhaa mbalimbali za maji nchini Tanzania na serikali ikiwa mmoja wa wateja wake wakubwa.

Akikabidhi cheti hicho, Ofisa wa Kampuni ya Bureau Veritas, Charles Vunugulu alisema kampuni hiyo imetimiza vigezo vyote ikiwamo kupitia mafunzo mbalimbali ya namna bora ya uendeshaji wa kampuni.

"Tutakachokifanya ni kuhakikisha kila baada ya mwaka tunafanya ukaguzi ili kuhakikisha kuwa kampuni inaendelea kuwa bora kila mwaka," alisema.

Kampuni ya Davis & Shirtliff inazalisha na kusambaza bidhaa mbalimbali ikiwamo pampu za maji, majenereta, mabwawa ya kuogelea, mashine za kutibu maji pamoja na mashine za umwagiliaji kwenye kilimo.




Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Davis & Shirtliff Tanzania, Benjamin Munyao (kushoto), akipokea cheti cha ubora cha Shirika la Kimataifa la ISO kutoka kwa Ofisa wa Kampuni ya Bureau Veritas, Charles Vunugulu (kulia), jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni wasimamizi na wakaguzi, Fausta Kusibago na Lizy Washuka. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# VETA yabuni maabara inayotembea kwa wanafunzi

**Elizabeth Zaya**

CHUO cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Chang'ombe kimebuni maabara ya kutembea ambayo itakuwa inafanya kazi kwa shule za sekondari na msingi zenye uhaba wa maabara hizo.

Akizungumza ndani ya banda la Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), kwenye Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) maarufu kama Sabasaba yaliyoanza Juni 28, mwaka huu, Mwalimu wa VETA Chang'ombe, Emmanuel Bakula, alisema tayari maabara hiyo imepewa kibali cha kuitumia katika shule ambazo zitahitaji.

"Maabara hii imetengenezwa mwaka jana mwaka huu ikapelekwa kwenye Maonyesho ya Mashindano ya Kisayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) ya mwaka huu na kushinda nafasi ya kwanza," alisema Bakula.

"Kwa hiyo iko tayari kwa matumizi na inaweza kwenda mahali popote itakapohitajika hasa kwa shule ambazo zina uhitaji na siziso na maabara au zenye maabara lakini hazina vifaa."

Alisema maabara hiyo inahuduma za mafunzo kwa vitendo zaidi kuhusu masomo ya sayansi ikiwamo fizikia.

"Na unaweza kuinunua kabisa na vifaa vyake ndani, pia huwa inakuwa na wataalamu wetu ambao ukiwahitaji wanafika popote kwa ajili ya kuwafundisha wanafunzi kupitia hii maabara," alisema Bakula.

Kwa upande wake mmoja wa wanafunzi walioshiriki katika kubuni maabara hiyo, Hawa Kitamba, alisema ubunifu huo utasaidia changamoto ya baadhi ya wanafunzi kutopenda masomo ya sayansi kutokana na ukosefu wa maabara.

Pia aliwashauri wanafunzi wa kike kupenda masomo ya sayansi kwa kuwa hayana ugumu wowote.

HABARI KITAIFA

# Moravian yamtathmini Rais Samia kwa siku 100

Na Beatrice Shayo

KANISA la Moravian Tanzania Usharika wa Tabata mkoani Dar es Salaam, limempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa utendaji wake kwa siku 100 alizodumu madarakani.

Mchungaji wa Kanisa hilo, Emanuel Mahembo, amesema kwa kipindi hicho amefanya mambo makubwa na mazuri na kwamba jambo la msingi ni kuwaombea wasaidizi wake ili asiingie doa.

Mahembo aliyasema hayo wakati wa ibada ya Sikukuu ya Umoja wa Wanawake wa kanisa hilo jijini Dar es Salaam, ambapo alieleza kuwa ndani ya siku 100 Rais Samia ameonyesha ujasiri kwa vitendo.

Alisema watawala wengi ambao wanazungukwa na washauri badala ya kusaidia watawala kuongoza vyema, wanafanya kinyume na matokeo yake wanaongoza vibaya.

"Tunamuombea Mungu ampe macho ya rohoni ili wanaomshauri wawe ni watu wema, kwa sababu sisi wa upande wa kanisa kuna nyaraka nyingi na vitu vingi tunajifunza... wapo watawala wengi ambao walizungukwa na washauri halafu washauri hao badala ya kusaidia watawala kuongoza vyema, wakajikuta wanaongoza vibaya," alisema.

Aliongeza: "Rais ameanza vizuri, Mungu amjalie apate wasaidizi walio waaminifu watakaomshauri vizuri na wasaidizi wake wasimame kwa uadilifu kutumikia nafasi zao ili Rais Samia asiingie doa katika utumishi alionao."

Aidha, alisema kwa siku 100 tangu Rais Samia alipoingia madarakani anaweza kuona ni kwa namna gani alivyoweza kuiongoza nchi.

Alisema kitendo cha Rais Samia kukubali kuongoza nchi, kinadhihirisha ni mwanamke jasiri na mwenye udhubutu na kujiamini.

Mchungaji alisema ni muhimu jamii ikatambua kuwa mwanamke anaongoza kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa, hivyo iondolewe dhana ya kuwaona wanawake hawawezi kushika nafasi kubwa za maamuzi.

Naye Makamu Mwenyekiti wa umoja huo, Prisiana Karumbo, alisema

wanamshukuru Mungu siku hii ya kinamama ya kanisa la Moravian imegongana na siku 100 za utendaji wa Rais Samia, ambaye ni kiongozi wa kwanza mwanamke Tanzania.



Mkurugenzi wa Uhusiano kwa Umma wa Kampuni ya Serengeti Breweries Ltd (SBL), John Wanyancha (kushoto), akizungumza, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa mpango maalum wa " Tunyanyuke Pamoja" wa kusaidia baa kupambana na magonjwa ya kuambukiza ikiwamo COVID-19 wenye thamani ya Sh. bilioni 2.3 kwa ajili ya kulinda afya za wateja na wahudumu. Wapili kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, Mwakilishi wa wamiliki wa Baa, Fredrick Mramba na Msambazaji wa Vinywaji, Kelvin Tegwa. **PICHA: JOHN BADI**

# DAWASA kuongeza mtandao wa majitaka

Na Crispin Gerald

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imesema itaongeza mtandao wa majitaka kutoka asilimia 14 ya sasa hadi 40 ifikapo mwaka 2025.

Akizungumza juu ya utekelezaji wa miradi ya uondoshaji majitaka majumbani, Meneja wa Miundombinu ya Majitaka wa DAWASA, Mhandisi Enock Mutalemwa, alisema utekelezaji wa miradi hiyo imelenga kuimarisha usafi wa mazingira na kupunguza uwezekano wa magonjwa ya mlipuko yanayosababishwa na utiririshaji wa majitaka.

"Kupitia idara ya majitaka tuna mipango mingi ya utekelezaji wa miradi ya majitaka ambayo inatekelezwa kupitia fedha za ndani za mamlaka na hadi sasa jumla ya miradi mitatu yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 350 imeshatekelezwa kuanzia Aprili hadi sasa," alisema Mutalemwa.

Alisema DAWASA imeongeza mtandao wa majitaka eneo la Sinza E katika mitaa ya Juma Ikangaa, Muungano na Imani na kazi hiyo imehusisha ulazaji mabomba ya ukubwa wa inchi nane kwa umbali wa kilomita 1.4 pamoja na mabomba ya maunganisho yenye urefu wa mita 581.

Kwa mujibu wa Mutalemwa, mradi wa Sinza kwa sasa uko kwenye hatua za maunganisho ya wateja wapya na kupitia mradi huo, wateja 100 wanategemea kuunganishwa kwenye mfumo wa majitaka.

# Wazalishaji, waagizaji vifungashio wafundwa

Na Mwandishi Wetu

MCHANGO wa wazalishaji, waagizaji na wasambazaji wa mifuko ya Non Woven na ya plastiki katika pato la taifa na upatikanaji wa ajira, utatokana na kuzalisha mifuko yenye kukubalika katika masoko.

Kukubalika kwenye masoko kunatokana na ubora unaokidhi matakwa ya viwango husika.

Hayo yalisemwa na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Lazaro Mwambole, wakati akifungua mafunzo ya wazalishaji, waagizaji na wasambazaji wa mifuko ya Non Woven na ya plastiki kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo, Dk. Yusuf Ngenya, jijini Dar es Salaam juzi.

Alisema TBS kwa kuunga mkono mipango na juhudi zote zinazofanywa na Serikali katika kukuza pato la taifa na kuongeza ajira kupitia sekta hiyo, ndiyo maana imekuwa ikitumia mamlaka iliyopewa ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinazouzwa zinazozalishwa nchini ikiwamo mifuko ya Non-woven bags, mifuko ya plastiki iliyoruhusiwa na sacks bags pia zinakidhi matakwa ya viwango.

"Kwa mantiki hiyo TBS itaendelea kutilia mkazo kusimamia masuala ya viwango na udhibiti ubora wa bidhaa," alisema Mwambole.

# TANAPA yawafikia wanafunzi 15,000 elimu ya uhifadhi

Na Alphonce Kabilondo, GEITA

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), limetoa elimu ya uhifadhi kwa wanafunzi wa shule za sekondari 5,500 na msingi 9,696 zilizopo jirani na hifadhi mbalimbali nchini.

Kamishna Msaidizi Kitengo cha Uhifadhi na Uhusiano wa Jamii (TANAPA), Godwell Meng'ataki, alisema hayo mkoani Geita wakati wa mafunzo ya kuwajengea wakuu wa shule za msingi na sekondari, maofisa elimu pamoja na wakurugenzi kutoka Halmashauri za Chato na Geita.

Alisema kati ya shule 22 walizowafikia wanafunzi kati yake 10 ni zilizojengwa na TANAPA kupitia mpango wa ujirani mwema.

Aidha, alibainisha kuwa walimu hao watakuwa na wajibu wa kutoa elimu ya uhifadhi kwa wanafunzi wa darasa la tano na saba kupitia masomo ya maarifa ya jamii, huku wakipendekeza masomo ya uhifadhi yaingizwe kwenye mtaala wa elimu.

Alisema kwa kipindi cha kuanzia mwezi Machi hadi Juni, mwaka huu wametoa elimu ya uhifadhi kwenye mikoa 10, wilaya 16, vijjji 66, shule 127 za msingi na maofisa wa serikali 207.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato, Eliudi Mwaiteleke, alisema anatamani elimu ya uhifadhi ianze kutolewa kwa wanafunzi wa darasa la tatu ili watakapohitimu wawe na uelewa mpana juu ya uhifadhi wa Hifadhi za Taifa.Naye Mkuu Wilaya ya Geita, Wilson Shimo, alisema bila kupambana na uharibifu wa mazingira upo uwezekano kupata madhara makubwa na kwamba kila mmoja kwa nafasi yake ana jukumu kupambana na uharibifu wa mazingira pamoja na hifadhi, huku akionya kuwa serikali haitasita kuchukua hatua kwa watakaobainika wakivamia maeneo yaliyohifadhiwa.

# Serikali yaweka msimamo kuhusu Mkomazi

SERIKALI imesema haina mpango wa kumega eneo la Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashid Shangazi. Katika swali lake, mbunge huyo alisema hifadhi hiyo imebana sana maeneo ya wananchi, hivyo kufanya kazi za kijamii katika kata za Lunguza, Mng'aro na Mnazi kushindwa kujiendeleza.

"Je, serikali haioni sasa ni wakati mwafaka kupunguza sehemu ya Hifadhi ya Taifa Mkomazi na kugawa kwa serikali za vijiji?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Masanja alisema Hifadhi ya Taifa Mkomazi imetokana na kupandishwa hadhi kwa lililokuwa Pori la Akiba la Mkomazi kupitia Tangazo la Serikali Namba 27 la mwaka 2008.

"Hifadhi hii ni sehemu ya mfumo wa ikolojia wa Tsavo-Mkomazi wenye wanyamapori wengi. Vilevile, ni maeneo ya mtawanyiko na shoroba za wanyamapori na tayari kumekuwa na changamoto nyingi za shughuli za binadamu katika maeneo hayo ambayo imesababisha kuwapo na migongano kati ya wanyamapori wakali na waharibifu (tembo) na wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi," alisema. Hata hivyo, alisema serikali haina mpango wa kumega eneo hilo kwa kuwa kuendelea kumega maeneo ya hifadhi ni kuendeleza migongano hiyo.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (kulia), akijadiliana jambo na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, ndani ya ukumbi wa Bunge jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ukaguzi waanza maeneo yasiyoendelezwa




WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imeanza ukaguzi wa maeneo yaliyomilikishwa kwa watu binafsi, wawekezaji wakubwa na mashirika ya umma katika mkoa wa Dar es Salaam.

Lengo la ukaguzi huo ni kubaini ukiukwaji wa masharti ya umiliki yaliyotolewa na kuanzisha taratibu za ubatilisho.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Angelina Mabula, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mbagala (CCM), Abdallah Chaurembo.

Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuyarudisha kwenye halmashauri maeneo yote yasiyoendelezwa na mashirika ya umma kwa zaidi ya miaka 10 ili halmashauri zijenge miundombinu ya huduma za jamii.

Akijibu swali hilo, Dk. Mabula alisema haki ya kumiliki ardhi hutolewa kwa mujibu wa sheria za ardhi na kwamba zimeweka masharti ya umiliki wa ardhi ikiwamo kufanya maendelezo ndani ya muda husika pamoja na hatua za kuchukua endapo kuna ukiukwaji wa masharti hayo.

Alikiri kwamba baadhi ya mashirika ya umma yaliyomilikishwa ardhi katika maeneo mbalimbali nchini hayajaendeleza ardhi zao.

"Katika kutatua changamoto hiyo, wizara kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kushughulikia ardhi iliyomilikishwa na kuachwa bila kuendelezwa," alisema.

Hata hivyo, alisema baada ya kubatilisha milki za maeneo ambayo hayajaendelezwa, ardhi husika hupangwa na kupimwa upya kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwamo uwekezaji, miundombinu ya huduma za jamii kwa kuzingatia mahitaji halisi ya sasa.

Alitoa rai kwa halmashauri zote nchini kuendelea kufanya ukaguzi wa maeneo yaliyotolewa kwa mashirika ya umma, kampuni na watu binafsi na kuanzisha taratibu za ubatilisho endapo itabainika uwapo wa ukiukwaji wa masharti ya umiliki na kuwasilisha mapendekezo wizarani kwa hatua stahiki.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alihoji lini wizara itakabidhi viwanja vya mradi wa viwanja 20,000 kwa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ili kupangia matumizi mengine maeneo yote ya taasisi ambayo hayakuendelezwa katika kata za Twangoma na Kibada ikiwamo mashamba pori ya NSSF.

Akijibu swali hilo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema mamlaka ya upangaji wa ardhi kwa mujibu wa sheria ni ya halmashauri na kwamba kwa Dar es Salaam kuna mradi ulianzishwa miaka ya nyuma wa viwanja 20,000.

"Leo (jana) nataka niseme hapa, viwanja vilivyopimwa 20,000 hasa vya Twangoma na Kibada nimeshaagiza na naagiza Wizara ya Ardhi ikabidhi michoro hiyo kwa Halmashauri ya Manispaa Temeke na wiki hii makabidhiano yafanyike. Wilaya ya Temeke isimamie ipasavyo mradi huu na ulikuwa mradi ndani ya wilaya ya Temeke na kama kuna ambao hawajaendeleza Temeke ni mamlaka kamili kutoa notisi kuchukua hatua na kuchukua ardhi hiyo," alisema.

# Ataka polisi vituo vya afya

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Husna Sekiboko, ameitaka serikali kuhamishia dawati la kijinsia kutoka Jeshi la Polisi kwenda vituo vya kutolea huduma za afya ili kusogeza huduma kwa wananchi.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alihoji lini serikali italeta mabadiliko ya sheria ili kutoa nafasi nzuri zaidi ya waathirika wa matukio ya ukatili kuyaripoti.

"Kwa kuwa vituo vya mkono kwa mkono ni vichache viko takribani 14 na tunahitaji kuwatunza wahanga (waathirika) wa matukio ya ukatili wakati wakisubiri mashauri yao kufanyiwa uchunguzi, serikali ina mpango gani kuongeza vituo hivi?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamisi, alisema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendeshwa kwa mujibu wa sheria mbalimbali.

"Jeshi la Polisi limepewa mamlaka kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Fungu 5 (322) ya mwaka 1965 na kuboreshwa mwaka 2002 ya kulinda raia na mali zake na kupeleleza makosa mbalimbali," alisema.

Hata hivyo, alisema dawati hilo ni vyema likaendelea kukaa lilipo sasa badala ya kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya.

"Katika kuhakikisha kuwa mwathirika wa vitendo vya ukatili wa kijinsia anapatiwa huduma rafiki na za haraka, dawati hili hushirikiana na vituo vya mkono kwa mkono (One Stop Centre) ambavyo viko kwenye vituo vya afya vikiwa na wataalamu wa afya, maofisa wa Jeshi la Polisi, ustawi wa jamii na wanasheria kwa ajili ya utoaji wa huduma stahiki," alisema.

ama
ALHAMISI JULAI 1, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Mustakabali 'A' hadi 'Z' katika ulingo afya, apatia tafsiri kitendawili corona**



Ukurasa 14

**ILIVYO MIKASA MIMBA ZAWANAFUNZI KAGERA NA AHUENI KURUDI DARASANI**

# SIKU 100 IKULU

## SERIKALI AWAMU YA SITA

# Bajeti yake juu, kiwanda dawa rasmi, vifaa tiba kwa wingi, bima afya yaja

**Na Yasmine Protace**



Rais Samia Suluhu Hassan, alipotembelea wagonjwa katika Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala. **PICHA: MAKTABA.**

WAKATI anachukua uongozi wa nchi ambao leo hii unatimu miezi mitatu kamili na nusu, bado kuna kumbukumbu ya tangu alipoapishwa, siku kadhaa baadaye na hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan, amedumu akiwahakikishia Watanzani kuwa yeye na mtangulizi, Hayati Dk. John Magufuli ni kitu kimoja.

Ni tafsiri inayoanzia dhana kwamba waliahidi umma, kupanga, kutekeleza na kuongoza pamoja, chini chini ya kivuli cha chama na ilani ya pamoja. Kwa lugha fupi, ni wanandugu waliojenga nyumba moja, kwa pamoja.

Muda si mrefu tangu kupata uongozi wa nchi, Rais Dk. Magufuli alifanya ziara katika Hospitali Kuu ya Taifa Muhimbili (MNH) na Bohari Kuu ya Dawa. Hapo ndipo akaibua haja ya nchi kujigharamia kuwa na kiwanda cha kuzalisha dawa.

Sura ya utekezaji wake sasa inashuhudiwa kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inapotangaza kutolewa fedha za kujenga kiwanda cha chenye uwezo wa kuzalisha dawa, kuchangia kuondoa uhaba wa dawa ulioumiza sana bajeti, kwa dawa kununuliwa kutoka nje ya nchi.

Ni hali inayotajwa kuwa na manufaa kwa hospitali binafsi na za umma, hapo kukishuhudiwa kushuka bei zake na wakati huohuo kusaidia ajira na pengo la bidhaa hiyo.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee a Watoto Dk. Godwin Mollel, anafafanua kuwa Rais Samia Suluhu Hassan, ameshatoa fedha za ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha dawa, ambacho kitakuwapo m mkoani Njombe, kikiwa na uwezo wa kuzalisha dawa za vidonge na vimiminika.

Anaeleza imani yake kuwa bei za dawa zitashuka, huku akijivuna kuwa hali ya huduma za afya inaendelea kuwa bora nchini, husan katika upatikanaji dawa.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri Dk. Mollel, serikali inaendelea kutenga fedha za kutosha kununua dawa na kwamba, serikali ilishatoa fedha jumla Sh. bilioni 123 kabla ya bajeti ya mwaka huu.

"Kwa kipindi kifupi cha Rais, mama yetu Samia Suluhu Hassan alivyoingia kwenye mamlaka, tumepata kiasi cha Sh. bilioni 123 kwa ajili ya dawa.

"Hizo ni fedha zilizotoka ndani ya muda mfupi kabla ya hii bajeti mpya ambayo tumeifanya, ambayo lengo lake ni kwenda kuimarisha suala la dawa, vifaa tiba na vitendanishi." anasema Dk. Mollel.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa jana bungeni, alipokuwa akikamilisha akiahirisha kikoa cha bunge jana, hali ya upatikanaji dawa, pia vifaa na vitendanishi ni nzuri sana kitaifa, viwanda vingi vya kutegeneza dawa na vifaa tiba vinaongezeka kwa kasi na vingine vinajengwa.

Waziri Mkuu anaziagiza kamati za Ulinzi na Usalama kufanya ajenda ya kudumu dhidi ya udokozi wa dawa hizo kila mahali.

Pia, Dk. Mollel anakiri kuwa serikali imekuwa ikipokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuhusiana na dawa, huku akiweka wazi tayari imeshamfikia Waziri wa Afya, Dk. Dorothy Gwajima.

Anasema ni mrejesho kutoka kwa timu ya ukaguzi aliyoichagua kwenda katika hospitali za mikoa na utekelezaji wake unaanza kudhibiti mianya yote ya upotevu wa dawa nchini.

Dk. Mollel anasema, serikali inaendelea kumalizia mchakato wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, utakaosaidia kila mwananchi kupata huduma bora katika vituo vyote vya kutoa huduma za afya, kuwarahisisha matibabu.

"Tukienda kuwa na Bima ya Afya kwa wote, maana yake kwenye eneo la afya tunaenda kufanya kila Mtanzania aweze kupata huduma bora za afya, lakini tunaenda kuondoa tatizo ambalo limekuwa likilalamikiwa siku zote la upatikanaji dawa liwe limetatulika.

"Serikali inapowekeza kwenye sekta nyingine, maana yake ni kwamba Sekta ya Afya nayo inaguswa moja kwa moja. Mfano Wizara ya Afya inapojipanga kupunguza vifo vya mama na mtoto, wakati mwingine inafika mahali tunagawa simu vijijini ili kuhakikisha uwapo wa mawasiliano ili kumuokoa mama mjamzito," anasema.



AFYA

# Mustakabali ‘A’ hadi ‘Z’ akiupa ulingo afya, aipatia tafsiri kitendawili corona

- Ajenda yake: Jiongeze Tuwavushe Salama
- Atia mguu Mwananyamala ‘tuko pamoja’
- Kuelekea Afya 2025 aanika ‘jambo lake’

**Na Mary Geofrey**



Rais Samia Suluhu Hassan, alipozungumza na kinamama jijini Dodoma hivi karibuni. Picha nyingine, ni umati wa kinamama walijojumuika naye katika ukumbi wa Jakaya Kikwete . **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

WATANZANIA wamekuwa wakisherehekea siku 100 tangu Rais Samia Suluhu Hassan, aapishwe Rais wa Tanzania, mnamo Machi 19, mwaka huu.

Ana mengi amegusa katika sekta nyingi kitaifa, afya nako si haba.

Katika hotuba yake ya kufungua Bunge, mjini Dodoma, Aprili 22, mwaka huu, anathibitisha serikali yake itaendelea kuimarisha na kuboresha huduma za jamii, hususan afya, elimu na maji.

Anataja kwamba, katika afya, ndani ya miaka mitano iliyopita yamepatikana mafanikio makubwa, ikiwamo kujenga vituo vya kutoa huduma za afya 1,887. Hapo kuna zahanati 1,198; vituo vya afya 487; hospitali za wilaya 99; hospitali za rufani za mikoa 10 na hospitali za rufaa za kanda.

**MWELEKEO 2025**

Mama Samia anahidi ifikapo mwaka 2025, serikali itaimarisha upatikanaji huduma za afya, kwa kuendelea kujenga miundombinu, kuongeza watumishi, vifaa tiba, dawa na vitendanishi.

Aidha, anasema juhudi za kupunguza vifo vya wajawazito na watoto zitaendelezwa, akinena: “Nilipokuwa Makamu wa Rais nilizindua kampeni ya ‘Jiongeze Tuwavushe Salama’ ili kutilia mkazo uwajibikiaji wa wadau wote katika kupunguza vifo vya mama na mtoto. Hivyo, huu ni mradi wangu wa moyoni kabisa.”

Anaeleza kusikitishwa kusikia mwanamke anapoteza maisha wakati wa kujifungua, kwa sababu zinazozuilika akiwa na ahadi serikali itaelekeza nguvu katika kinga na tiba, ikiwamo kwa magonjwa yasiyoambukiza yanayosababisha vifo vingi na kuigharimu serikali fedha nyingi.

“Tutaimarisha, pia huduma za matibabu ya kibingwa na kuzipeleka huduma hizi kwenye hospitali za rufani za mikoa. Tutaimarisha utoaji huduma za matibabu kwa wazee, na kutaweka mipango maalum kuhudumia makundi yenye magonjwa adimu,” anasema Rais Samia.

Anahimiza serikali itaimarisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kufikia lengo la ‘Bima ya Afya kwa Wote’ na kwa sasa kuna watu 8,224,271 sawa na asilimia 14 ya Watanzania ndio wanaotumia bima ya afya.

“Vilevile, tutahamasisha ujenzi wa viwanda vya kutengeneza dawa, vitenganishi, vifaa tiba pamoja na chanjo mbali mbali,” anasema Rais Samia.

**CORONA JE?**

Kuhusu ugonjwa corona, anakiri umeathiri dunia nzima, nchini ikiwa na namna ya kuja na kuondoka katika mifumo tofauti na mpaka sasa hakujawa na dalili za kupatikana tiba sahihi.

Rais Samia anataja njia pekee iliyopo ni kujikinga na kuchukua hatua mbalimbali za tahadhari. Rais Samia anaendeleza kauli:

“Hapa nchini tumekuwa tukifuata miongozo kadhaa ya kinga inayotolewa na wataalamu kwa kutumia njia zetu za tiba asilia. Tumeweza kwa kiasi kikubwa kushusha kiwango cha maambukizi.”

Pia, anaeleza serikali imeunda Kamati ya Wataalamu ambao kwa kushirikiana na taasisi za afya duniani na kikanda kama Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Rais Samia analichabua hilo kwa undani na kulichambua, kisha mapendekezo yanatolewa kuhusu haja ya kuendelea kupambana na maradhi hayo.

Kiongozi mkuu huyo wa nchi, mnamo Mei 14, mwaka huu akiwa katika Baraza la Iddi lililofanyika mkoani Dar es Salaam, alisisitiza serikali itajiridhisha kuhusu chanjo zinazotolewa na mataifa mengine, kabla ya kuamua.

“Nataka kuhakikishia kwamba tahadhari mlizitoa juu ya chanjo na mengine zitafuatwa kikamilifu na serikali yenu, Hata hivyo, hii haina maana kwamba tutapokea kila kitu tunacholetewa au kuambiwa la hasha, lazima na sisi tujiridhishe kwa hiyo.

“Hata suala la chanjo nalo tutajiridhisha kabla ya kuamua kutumia au kuacha kutumia. Hivyo, nawasihi Watanzania kutokuwa na hofu yoyote, serikali ipo makini katika kushughulikia suala hilo,” anathibitisha Rais Samia.

**MTAZAMO KISERA**

Katika siku 100 za utawala wa Rais Samia, anahimiza uvaaji barakoa ana kujilinda, huku serikali imekubali kufuata ushauri wa kitaalamu nchini, ikwamo kupokea chanjo za corona , kwa hiari za raia wake, huku tiba asilia zikiendelea kutumika.

Rais Samia anaeleza imani yake katika anachokitaja ‘ukitaka kufika mbali, uende na wenzako.’ Hivyo, serikali imekubali kujiunga na harakati za dunia katika mapambano dhidi yake.

**MWANANYAMALA HOSPITALI**

Juni Mosi, mwaka huu, Rais Samia alitembelea Hospitali ya Rufani Mwananyamala Dar es Salaam, alikowasisitiza wananchi kuendeleakuchukua tahadhari ya kujikinga dhidi ya virusi vya corona, kwa kuzingatia uvaaji barakoa hata katika mazingira salama.

Akiwa hospitali humo, Rais Samia alizuru wodini kuwapa pole wagonjwa waliolazwa na zawadi ya mashuka 200 akiwaachia salamu:“Leo Mama yenu nimekuja na mashuka 200 ili wagonjwa walale pazuri.

“Mara nyingine nitakuja na zawadi kubwa, zawadi nyingine nakwenda kuangalia maslahi yenu watumishi, jinsi uchumi utakavyoniruhusu nitawawekea mambo mazuri ila ili uchumi ukue tuchape kazi.

“Nimetoa zawadi ya mashuka 200 ili wagonjwa walale pazuri, mkikuta mashuka yamechanikachanika wagonjwa wamelazwa pigeni kelele tusikie kwasababu mashuka 200 si haba pamoja na waliyonayo wapate kubadilisha, la upungufu wa dawa nitalishughulikia.”

**MJADALA NA WAHARIRI**

Jumatatu ilioyopita aliwaambia wahariri wa vyombo vya habari Ikulu Dar es Salaam, kwamba kuna wagonjwa wastani 100 na kati yao 70 hali yao siyo nzuri, wanapumulia kutumia oksijeni.

Rais Samia anasisitiza kuwa Wimbi la Tatu la Corona linaendelea kusumbua mataifa mengi duniani, ikwamo Tanzania, hivyo anawataka wananchi kuchukua tahadhari kama inavyoshauriwa na wataalamu.

Anasema, tayari serikali imeshatuma maombi ya kujiunga na Mpango wa Uagizaji Chanjo Kwa Nchi Zenye Uchumi Mdogo wa COVAX.

Kwa mujibu wa Mama Samia, kujiunga na mpango huo ni sehemu ya mapendekezo yaliyotolewa na kamati aliyoiunda, siku chache baada ya kuingia madarakani.

“Ilibidi tutume maombi ya kujiunga na COVAX kabla ya Juni 15, ili tuweze kupata chanjo kufikia mwaka 2022. Kwa waliochelewa kutuma maombi mpaka tarehe hiyo, maana yake wataingizwa kwenye mpango huo kufikia mwaka 2023. Kwa hiyo, tuliona kwanza tujiunge na mpango....,” anaeleza Rais Samia.

Mkuu wa WHO, mmoja ya waratibu wakuu wa COVAX kwa Kanda ya Afrika, Dk. Matshidisi Moeti, hivi karibuni alinukuliwa kuwa chanjo zinaweza kuingia Tanzania ndani ya wiki kadhaa baada ya kujiunga rasmi.

Juni 17, mwaka huu, WHO lilikiri kupokea taarifa rasmi ya Tanzania kuomba kujiunga na mpango wa COVAX unaolenga kuhakikisha nchi masikini kote duniani zinapata mgao sawa wa chanjo.

Mkuu wa WHO Kanda ya Afrika Dk. Matshidiso Moeti, amenukuliwa akisema kuwa chanjo hizo zinaweza kuingia Tanzania katika kipindi cha wiki mbili.

Namna gani itatumika? Rais Samia anafafanua kuwa, wamekubaliana katika Baraza la Mawaziri, chanjo hiyo itakuwa ya hiari, kama ulivyo mfumo wa dunia na hakuna kulazimishana.

Pia, Rais Samia anasema kuna mashirika ya kimataifa na baadhi ya nchi zimeshajitolea kuipa Tanzania msaada wa chanjo. Hata hivyo, anasisitiza kwa angalizo: “Huu hautakua msaada tu wa kupokea, lazima wataalamu wetu wazikague chanjo hizo na kutushauri kabla ya kuzipokea.”

Mnamo Juni 10, mwaka huu, Shirika la Fedha Duniani (IMF) lilithibitisha litaipatia Tanzania mkopo wa dharura wa Dola za Marekani milioni 574, itakapokamilisha mambo muhimu yahusuyo corona.

Mara ya mwisho Tanzania kutoa takwimu kuhusu maambukizi ya virusi hivyo na ugonjwa wa Covid 19 kwa ujumla ilikuwa Mei, mwaka 2020.





MAZINGIRA

# Rais Samia anavyoushika mpini 'iwe isiwe' huduma maji iwafikie wahitaji

- Siku uteuzi: Waziri 'ukinizingua nitakuzingua'
- Mainjinia lao laja; mradi Misungwi kwa 64,000

**Na Renatha Msungu, DODOMA**



Rais Samia Suluhu Hassan, alipozindua mradi mkubwa wa maji wilayani Misungwi, Mwanza.

MWISHONI mwa wiki iliyopita, Rais Samia Suluhu Hassan, ametimiza siku 100 katika uongozi na inahesabu siku ya 105. Baada ya tathmini ya kilichojiri katika Sekta ya Ardhi wiki iliyopita, iliyoadhimishwa Wiki ya Utumishi wa Umma hadi Mei 23, ikioanishwa na utawala wa Rais Samia Suluhu Hassan. Leo inahusu Wizara ya Maji.

**USHUHUDA WA RAIS**

Sekta ya Maji, ni eneo mojawapo Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa akifuatilia kwa karibu hata kukemea ambacho hajaridhika katika utendaji wao, hata akatoa angalizo kwa baadhi ya maofisa kimkoa.

Katika kauli yake kukemea moja ya hotuba zake kwa waziri mwenye dhamana na maji, Rais Samia akatamka kwa ukali usemi aliyoubebesha umaarufu "...ukinizungua, nitakuzingua..." ikiwa ishara ya kutoridhika na utendaji wake.

Ndani ya ziara zake kuwatembelea wananchi, alikagua huduma za maji nchini. Rais Samia Suluhu Hassan, ameshudia kinachofanywa na mabadiliko ya mapinduzi yanayofanyika katika sekta ya maji, sambamba na kuwahakikishia wananchi majisafi, salama na yanayotosheleza mahitaji.

Alipokuwa ziarani jijini Mwanza, Rais Samia, moja ya kazi aliyofanya ni kuzindua Mradi wa Maji wa Misungwi wenye thamani ya Sh. bilion 13.77 watekelezaji wake wakiwa serikali na wabia wa maendeleo.

Kauli yake kwa mamia ya wakazi walioshuhudia uzinduzi huo wilayani Misungwi, Rais Samia, anawataka kulinda miundombinu ya maji iliyojengwa nchini, kwa sababu serikali imeingia gharama kubwa kuitekeleza ili kufikisha huduma ya majisafi na salama kwa jamii.

Rais Samia ameiagiza wizara na Wahandisi wa Mkoa na Wilaya jijini Mwanza kuhakikisha maji yanasambazwa kwa kasi sana ili yawafikie wananchi wote na kuongeza mazingira yalindwe ili kulinda vyanzo vya maji.

Katika hili anawasihi wananchi kujenga tabia na utaratibu wa kuvuna maji ya mvua kwa kujenga mabwawa na visima, ili kuchangia kumaliza tatizo hilo kwa umma nchini.

Sambamba na hilo, anawataka wananchi kulipa bili za maji kama namna ya kuifanya huduma, hivyo kuwa endelevu na kufikishwa kwa wananchi wengine wahitaji.

Rais hakuwa na simile anapoipa angalizo Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza (MWAUWASA) 'kutokubambikizia' wateja bili za maji za mwezi bali, bali ziendane na matumizi halali, huku akitoa angalizo kwa upande wa pili, watumiaji nao wawajibike kulipa kwa wakati.

**WAZIRI AWESO**

Jumaa Aweso, Waziri wa Maji aliyepewa angalizo "akizingua, atazinguliwa" anatumia hafla ya uzinduzi, kuwajibuika mbele ya mkuu wa nchi, akiwaambia wananchi hao mageuzi yanayofanyika katika sekta yake, inalenga kuwahakikisha wanapatiwa majisafi, salama na yanayojitosheleza

Anasema jambo la msingi kwao ni kumpa ushirikiano wa kutosha Rais, ili dhamira ya kuleta maendeleo kwa wananchi itimie kama ilivyopangwa.

"Maji ni uhai na maji hayana mbadala. Kwa mfano, ukilinganisha na chakula, kwamba ukikosa wali basi utakula ugali,"anatamka katika msisitizo wake.

Anaendeleza hoja kwa msemo "anayejua mihemo ya mgonjwa ni yule aliyelala naye" hivyo mipango yote kiserikali ni kuhakikisha maji yanatoka bombani, kero kwa kinamama na ndoo na jamii kwa ujumla ifutike.

**KIWANGO CHA MAJI**

Waziri Aweso anasema, serikali ilianzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), inayohusika na ujenzi, pia miradi na usimamizi wa huduma ya maji vijijini, ukirithi miradi yote ya maji kitaifa.

Anasema baadhi ya miradi iliyorithiwa, imekuwa na matatizo ya kutokamilika kwa wakati na mingine imekamilika bila ya kutoa maji, akizijumuisha jumla yao miradi 177.

Kwa mujibu wa Waziri Aweso, hadi kuifka Machi 2021, kuna miradi 85 ilipatiwa ufumbuzi na kuanza kutoa huduma ya maji.Anaorodhesha mifano kuwa ni miradi ya Ntomoko(Dodoma); Nyamtukuza ( Geita); Mibono (Tabora); Rugeye (Mwanza); Malinyi ( Morogoro); Muze Group (Rukwa); Kinesi ( Mara) na Imalabupina-Ichwankima ya Geita.

Aweso anasema kuongezeka kazi za kuibua tena miradi hiyo iliyochechemea inaendelea kwa kutumia timu maalum za wataalamu, zilizopewa jina "Water Rescue Teams"

Waziri Aweso anatamba na anachokiita 'mapinduzi na mageuzi makubwa yaliyojiri katika Sekta ya Maji"

ni pamoja na kuzinduliwa miradi mikubwa ya maji ya Tabora, Igunga, Nzega, Isaka na Kagongwa. Hiyo ni baada ya kazi kubwa ya utekelezaji wake kukamilika.

Aweso anataja utekelezaji mwingine mbali na miradi 85 iliyokuwa na changamoto ya kukamilika, ipo miradi 422 ya maji katika mgawanyo 355 inagusa vijijini na 67 mijini.

Pia, waziri anataja wastani wa miradi 150 ya maji inayoendeshwa kwa gharama nafuu, pasipo kutumia makandarasi maarufu 'Force Account'

Ndani ya mageuzi hayo, pia kuna nyongeza ya idadi ya maabara za ubora wa maji zenye ithibati zinazotumika kupima ubora wa maji kufikia kiwango cha kimataifa.



Waziri Jumaa Aweso, alipozindua mradi wa maji mkoani Katavi, alipokuwa Naibu Waziri wa Maji, mwaka jana. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**KATIBU MKUU**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, anaeleza kuwa Mradi wa Maji wa Misungwi, una uwezo wa kuzalisha kwa siku lita milioni 4.5 zinazoweza kuhudumia wananchi 64,000 wa Misungwi na jirani.

Mhandisi Sanga, anasema Mradi wa Maji Misungwi wenye mabomba urefu wa kilomita 57.14 yameongeza upatikanaji maji, kutoka asilimia 42 hadi 83 huko Misungwi Mjini.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Robert Gabriel, anasema wastani wa upatikanaji huduma ya majisafi mkoani, uko asilimia73 na inazidi kuimarishwa kuelekea malengo yaliyowekwa na serikali.

**HALI YA MAJI**

Kulingana na takwimu zilizopo, huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini na mijini hadi kufikia Machi, mwaka huu imepanda vijijini ikiwa asilimia 72.3 kutoka asilimia 70.1.

Pia, katika kipindi hicho upatikanaji majisafi imeongezeka kutoka asilimia 84 mnamo Machi mwaka jana hadi asilimia 86 kipindi kama hicho mwaka huu.

Takwimu kutoka tafiti zilizofanywa na Wizara ya Maji mwaka 2019, zinaonyesha rasilimali za maji zinazoweza kupatikana kwa ajili ya matumizi kwa mwaka ni mita za

ujazo bilioni 126, kati yake mita za ujazo ni bilioni 105 ni maji juu ya ardhi na mita za ujazo bilioni 21 za maji chini ya ardhi.

Kwa kurejea makadirio ya idadi ya watu milioni 55.9 waliopo nchini kwa mwaka 2019, kulikuwapo wastani wa

Mita za ujazo wa maji 2,250 kwa kila mtu, wakati wastani wa matumizi ni mita za ujazo 1,700, ambacho ni kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kila mwaka, kinachokubalika kimataifa.

Hapo ndipo kuna rai ya Rais Samia Suluhu Hassan, katika haja ya jamii kwa jumla kuthamini kutunza mazingira, ili yanufaishe vizazi vya sasa na vijavyo, hali kadhalia, maji yataendelea kupatokana kwa wingi.



AFYA

# ILIVYO MIKASA MIMBA ZA WANAFUNZI KAGERA NA AHUENI KURUDI DARASANI

## •Aliyekutwa nayo asimulia machungu

**Na Lilian Lugakingira, ALIYEKUWA MULEBA**

"ALINIPA lifti wakati natoka shule akanipeleka hadi nyumbani. Tangu siku hiyo, tukazoeana akawa ananibeba mara kwa mara katika gari lake.

"Nikashawishika na kumkubalia, ndiyo chanzo cha kupata mimba na kufukuzwa shule," Ainath (Jina la pili tunalo), ana simulizi kutoka makazi yake, Magata, wilayani Muleba, mkoa Kagera.

Mzazi huyo mwenye umri miaka 20, sasa ana mtoto wa mwaka mmoja na miezi miwili. Alipata ujauzito kidato cha nne iliyompotezea ndoto ya baadaye kuwa mwanasheria au hakimu.

Anasimulia chimbuko ni kijana mwendesha magari ya abiria aliyefahamu anakoishi na alimtembelea kila mara, hata akashawishika kuingia kwenye uhusiano wa kimapenzi.

"Baba yangu wakati huo alinikasirikia, nilimwomba msamaha akanisamehe na sasa ananisaidia kutunza mtoto wangu wa kike, kwa kile kidogo anachokipata," anasema, huku akigusa upande wa pili, tangu mkasa hajawamuona tena mwenza.

Ainath anasema, kwa sasa anaishi kwa bibi yake mzaa mama, baada ya mama mzazi kufariki, akikumbuka ugumu wa mwanafunzi kubeba ujauzito, kwani anakosa mwelekeo kimaisha, hata anaposamehewa kuanza maisha mapya.

"Ombi langu nipate mtu wa kunishika mkono nijiendeleze kimasomo au likishindikana hilo nipate mtaji kidogo niweze kumtunza mwanangu ambaye baba yake alikimbia kukwepa mkono wa sheria" anasema.

Anakiri hadi ujauzito wake, hakumfahamu ndugu yeyote wa mwenza anayedai kwao ni mjini Bukoba. Sasa anaasa:"Sitaki wenzangu waangamie wala wapitie mateso niliyopitia, nawashauri wasome wasidanganyike, maana masuala ya mahusiano hayaishi hata wakimaliza shule watayakuta."

**MRATIBU DINI**

Magreth Kyabona, Mratibu wa Umoja wa Mama wa Kikristo katika Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Lweru Muleba, anafafanua:"Mmomonyoko wa maadili katika jamii unachangia kwa kiwango kikubwa tatizo hili, kulingana na mila na desturi kihistoria.

"Zamani mtoto alikuwa wa wote na ndiyo maana alipokutwa akifanya kosa aliadhibiwa na mtu mzima yeyote tena usingesikia manung'uniko.

"Mzazi wa sasa bila kujali kwamba jirani aliyemwadhibu mtoto wake alilenga kumfundisha mambo muhimu yatakayomfaa maishani, anakwenda polisi kushtaki kuwa mwanawe kapigwa na kuumizwa. Hali hii inaifanya jamii kuona mtoto anafanya mambo yasiyofaa na kukaa kimya," anafafanua.



Kaimu Ofisa Elimu Sekondari Wilaya ya Muleba, Godlove Ngirwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Anatoa mfano, simulizi ya namna jirani anavyoweza kukuta mtoto anafanya kosa bila ya kuepuka msuguano, anajiweka mbali hata kama ameona mzigo wa ulezi wakiachiwa walimu.

"Mtoto akiamka asubuhi, anakwenda shule, atarudi nyumbani jioni na akifika atawakuta wazazi wake wako 'bize' na maisha, hawana hata muda wa kukaa na kuwasikiliza watoto," anasema.

Anaendeleza tathmini ya upande wa pili kwamba watoto nao wakishatambua haki hiyo hubaki kimya na yao rohoni, matokeo yake wanaangukia matendo yasiyofaa, ikiwamo uhusiano ya kimapenzi.

Magreth anaendelea: "Hali hii huwafanya watoto kuvutiwa zaidi na mambo ya kisasa zaidi ya mambo ya kiroho."

Anafafanua kwamba kinamama ndiyo wanaokaa na watoto muda mrefu na ana hushauri zifanyike semina vijijini za kuwafundisha malezi ya watoto na faida zake katika maadili bora ya kuwasikiliza na kutatua magumu yao kabla ya kutokea madhara.

Mama huyo anapinga kuwapo wazazi wanapomuona mtoto anapotoka kidogo, wanaweka tafsiri safi tena ikiwamo mbadala wa malezi inayojumuisha kumjengea hofu mtoto

"Mzazi anapaswa kumwomba Mungu ampe hekima ya namna ya kuzungumza na mtoto wake, maana kama amekwishaanza kupotea anaweza kubadilika kupitia mafundisho na kumwomba Mungu," anasema.

Pia, anataja kuwapo baadhi ya watoto waliokata tamaa kutokana na ukali wa wazazi na wanaishia kuwakimbia na ndio mwanzo wa mimba na kaka zao kuangukia dawa za kulevya.

**OFISA ELIMU**

Godlove Ngirwa, Ofisa Elimu Taaluma akimuwakilisha Ofisa Elimu Sekondari wilayani Muleba, anasema mimba zimeshuka kati ya Januari na Aprili mwaka huu, wanafunzi wanne kulinganisha na wastani 15 hadi 20.

Anasema mwaka 2019 kulikuwapo mimba 25 na mwaka 2020 walikuwapo 15. Anafafanua:"Kilichosababisha mimba kupungua shuleni, baada ya mkuu wetu wa wilaya Mhandisi Richard Ruyango kutoridhishwa na hali hiyo aliunda kamati ya kudhibiti mimba na utoro shuleni."

Ngirwa anasema, kamati hiyo imekuwa ikifuatilia wanafunzi kwa karibu na kuwachukulia hatua wanaobainika kuhusika na mimba za wanafunzi.

"Kama kuna mtoto kapewa mimba na ikabainika kuna mambo yanafichwa, kamati imekuwa ikinyanyuka na kwenda kufuatilia na kuhakikisha kama kuna mtuhumiwa hajakamatwa basi atafutwe na akipatikana achukuliwe hatua za kisheria" anasema.

Anataja yanayochangia mimba shuleni yanajumuisha malezi duni ya wazazi, watoto kukosa matumizi kutoka kwa wazazi, kusababishwa waanze kutafuta wanachokihitaji, ilhali hawajitambui, jambo linalowafanya kila wanapokutana na wajanja wanadanganyika kirahisi.

"Kabla ya kamati hii kuundwa, watoto waliokuwa wakipata mimba shuleni walikuwa zaidi ya 100 kwa mwaka, lakini sasa idadi hiyo imepungua na kufikia watoto 15 kwa mwaka 2020," anasema Ngirwa.

Anasema, kinachofanyika sasa ni serikali inahimiza jamii zianzishe miradi kama ya kujenga mabweni, kwa lengo la kuwezesha sehemu kubwa ya watoto na hasa wasichana waishi shuleni, kuepuka vikwazo vya njiani.

"Mwanafunzi kubeba mimba sio kwamba ndiyo amepotea kabisa kimaisha. Hili linaweza kuwasaidia kutimiza ndoto zao, lakini linaweza kuwa funzo kwa wengine na kuwaepusha kujiingiza katika vitendo hivyo.

"Maana changamoto anazokumbana nazo za kusoma akiwa mama ni kubwa, ikiwamo kupoteza muda na kunyanyapaliwa," anasema.

**PROFESA KATIBU TAWALA**

Profesa Faustine Kamuzora, Katibu Tawala wa Mkoa Kagera, anasema serikali imepunguza mimba shuleni na zaidi zinasababishwa na ukosefu wa elimu ya uzazi shuleni na sehemu kubwa ya waathirika ni wasiojitambua.

"Pia itasaidia watoto wa kiume kujua miili yao inavyofanya kazi na mabadiliko ya kibailojia, kama tunataka kuondokana na mimba shuleni haya yasionewe aibu," anafafanua.

**MKURUGENZI WA LHRC**

Anna Henga, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu nchini (LHRC), anasema utekelezaji haki unaendana na utashi wa kisiasa kuhakikishia mtoto mwanzo wake na hasa elimu.

"Kama serikali imeanza kuangalia namna watoto hao watakavyorudi shule, sisi tunaona ni jambo la kushangiliwa, maana changamoto ya watoto wa kike kupata mimba na kushindwa kuendelea na masomo ni kubwa," anasema na kuongeza

"Ni mtoto, anapokosea na unapomnyima elimu unakuwa hujamrekebisha, maana mtoto inabidi anapokosea angalau apewe nafasi ya pili kumrekebisha.

Anasema LHRC inaunga mkono hatua hiyo na ili watoto waweze kurudi shuleni, wao watetezi wa haki za binadamu wana mtazamo:

"Hata kama tunatetea haki za binadamu sio kwamba tunafurahishwa na vitendo vya wanafunzi kubeba mimba wakiwa shuleni. Nawashauri wasome kwa bidii ili waepuke vishawishi."

**WAZIRI NDALICHAKO**

Hivi karibuni mwenye dhmana na elimu, Profesa Joyce Ndalichako, anasema serikali imeweka utaratibu utakaowezesha watoto watakaopata ujauzito shuleni, kuendelea na masomo kupitia elimu mbadala.

Profesa Ndalichako anasema wanafunzi hao wanaweza kuendelea na masomo kulingana na uhalisia wa ngazi aliyokwama. Anaendeleza kwa mfano: "Akipata mimba akiwa katika kidato cha kwanza, anaweza kupitia katika mfumo huo wa elimu mbadala na akifika kidato cha pili akafaulu mtihani anaweze kurudi katika mfumo wa kawaida.

Anaendelea: "Aliyeacha shule kidato cha tatu anafanya mtihani katika mfumo usio rasmi wa kidato cha nne na anapofaulu, anapangiwa nafasi ya masomo ya juu, kulingana na ufaulu wake."



Mwanafunzi Olvia, aliyepata mimba shuleni.





# Msajili ataka wanawake kutoa maoni mabadiliko sheria vyama

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Msajili wa Vyama vya Siasa, Mohamed Ally Ahmed, amewashauri wanawake kuwasilisha maoni yao kwa ajili ya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ili kuongeza ushiriki wao kwenye nafasi za uongozi.

Ahmed aliyasema hayo jana kwenye mkutano wa wadau wa vyama vya siasa, Ofisi ya Msajili wa Vyama na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), wenye lengo la kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi ili kufikia uwiano wa 50 kwa 50.

Mkutano huo uliandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) kwa kushirikiana na Kituo cha Usuluhishi (CRC) na Young & Alive Initiative (YAI) kwa ufadhili wa Shirika la Kihabari la Femnet.

"Kwa sasa tuko kwenye mchakato wa kurekebisha sheria yetu. Sisi kila baada ya uchaguzi tunapitia sheria na wakati wa mchakato huwa tunapelekea wadau wetu ili kutoa maoni yao kuona vitu vya kuongezwa," alisema.

Naibu Msajili huyo alisema kama wanawake wanaona kuna vitu vyenye tija kwao havipo kwenye sheria ya sasa, watumie fursa hiyo kutoa maoni yanayolenga kumwongezea mwanamke fursa ya kuwania uongozi.

"Mkitusaidia mawazo haya mtakuwa mmesaidia taifa hili. Kuna usemi kwamba ukimwelimisha mwanamke umeelimisha jamii, kwa kuwa ndio wanaokaa na familia," alisema.

Hata hivyo, alisema sheria hiyo kwa sasa inampa fursa mwanamke wa kitanzania kushiriki katika kuwania uongozi.

"Sheria ya vyama vya siasa iko wazi inasema chama chochote cha siasa lazima kinapotengeneza ilani au katiba yake, kihakikishe zizingatie usawa wa kijinsia bila ubaguzi wowote wa masuala ya jinsia," alisema na kusisitiza kuwa wanawake wanapaswa kuwa na fursa sawa na wanaume kupata nafasi za uongozi.

"Kumekuwa na changamoto kama mnavyoelewa. Wanawake kwa muda mrefu wamekuwa nyuma sasa ukiweka kwamba unatoa fursa sawa kwa mujibu wa sheria, lakini hujaweka mazingira ya kuhakikisha vile vyama vinaionyesha fursa kiuhalisia," alisema.

Alisema kuna uwezekano wa kukosa idadi ya wanawake waliopiganiwa kuwania uongozi kupitia sheria hiyo.

Alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa fursa mbalimbali anazowapa wanawake ambao wamekuwa chachu ya kuwahimiza wanawake wengine kushiriki katika masuala mbalimbali ya kisiasa.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Rose Reuben, alisema asilimia 51 ya watu nchini ni wanawake lakini ushiriki wao ni mdogo katika siasa na uongozi na kwamba wakihimizwa itasaidia kupiga hatua.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Bungeni (TWPG), Shally Raymond, alipendekeza NEC kuweka kanuni ambayo itatoa adhabu ikiwamo kuwaengua wagombea watakaowanyanyasa au kuwadhalilisha wagombea wanawake.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa (katikati), akipiga makofi wakati wa uzinduzi wa mfumo wa mtandao wa "Sema na Waziri wa Utumishi" kwa ajili ya kupokea malalamiko ya watumishi wa umma, jijini Dodoma juzi. Kulia kwake ni Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Deogratius Ndejembi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Joto kali chanzo cha mazao hafifu samaki

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imesema joto likiongezeka hadi kufikia nyuzi joto 70-90, malisho ya samaki yajulikanayo kama matumbao baharini hupotea na kupunguza uzalishaji wa samaki.

Mkurugenzi wa Utafiti wa TMA, Dk. Ladislaus Chang'a, aliyasema hayo juzi katika warsha iliyoandaliwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa watafiti kutoka taasisi za afya, maliasili, kilimo na mifugo.

Dk. Chang'a alisema hali hiyo itasababisha samaki kushindwa kuzaliana kutokana na kukosa chakula.

"Tunatakiwa kuwa makini na taarifa zinazotolewa na TMA ili kujua nini kinaendelea," alisema Dk. Chang'a.

Alisema viashiria vingine vya mabadiliko ya hali ya hewa ni kwamba joto la chini litaongezeka zaidi kuliko la juu, matukio ya hali mbaya ya hewa ikiwamo ya ukame, mafuriko, mvua kubwa na upepo mkali vimeendelea kuongezeka na kuathiri sekta zote kiuchumi.

Kutokana na hali hiyo, alizishauri sekta hizo kujenga tabia ya kutumia taarifa mbalimbali zinazotolewa na TMA ili kujua mabadiliko ya hali ya hewa yanayojitokeza pamoja na athari zake zitakazowawezesha kuchukua tahadhari ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza.

Alisema endapo kasi ya mabadiliko ya hewa yataendelea kuongezeka, joto nalo likiongezeka hadi kufikia nyuzi joto 1.5 duniani kati ya mwaka 2030 na 2052.

Dk. Chang'a alisema katika ongezeko hilo nchi zinazoendelea zitaathirika zaidi kutokana na kuwa na uwezo mdogo wa kuhimili athari hizo za mabadiliko ya hali ya hewa.

Alifafanua kuwa kati ya mwaka 2015, 2018, 2019 na 2020 hali ya joto ilikuwa nyuzi joto 1.2 ambacho kilikuwa ni kiwango cha juu tofauti na ilivyo kawaida.

# Waziri aonya maofisa biashara kufunga maduka

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Geofrey Mwambe, amewataka maofisa biashara kuacha tabia ya kufunga maduka ya wafanyabiashara wanaodaiwa kwa kuwa ni kuhujumu uchumi.

Pia amesema kuna haja ya kufanyika mabadiliko katika usimamizi wa fedha za asilimia 10 zinazotolewa na halmashauri kwa vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Mwambe aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua kikao cha maelekezo kwa maofisa biashara wa mikoa kilichoandaliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

"Lazima hili nyie ndio mlisimamie na si maofisa maendeleo ya jamii kwani wao hawafahamu chochote kuhusu biashara. Wanachotakiwa kufanya ni kusajili vikundi na kuhakikisha vinapata mikopo," alisema Mwambe. Alisema kuwatumia maofisa maendeleo ya jamii kusimamia mikopo hiyo ya asilimia 10, kutasababisha vikundi vingi kushindwa kupiga hatua kutokana na kukosa wataalamu wa masuala ya biashara.

Akizungumzia vitendo vya maofisa biashara kufunga maduka ya wafanyabiashara kutokana na kudaiwa mapato au kuisha kwa leseni alisema si jambo la busara.

"Unakuta mtu anadaiwa fedha kiasi kidogo tuu labda leseni yake imeisha siku chache zilizopita lakini ofisa biashara anafunga duka na kufuri. Jambo hili ni sawa na ilivyo katika kosa la uhujumu uchumi," alisema Mwambe.

Aidha, alisema badala ya maofisa biashara kufunga makufuri maduka, watumie busara kwa kuwaita na kukaa nao meza moja ili kujadili namna bora ya kulipa madeni yao.

Pia aliwataka maofisa kuacha urasimu katika mikoa yao pindi wanapojitokeza wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza katika sekta mbalimbali.

"Ili kuvutia wawekezaji tunahitaji kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji kwa kuandaa vibali kwa wakati lakini pia kuendeleza rasilimali watu," alisema. Kadhalika, alisema ofisi yake kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na Ofisi ya Rais Utumishi, wako katika mchakato wa kuundaa idara ya biashara katika mikoa ili ijitegemee katika utekelezaji wa majukumu yake.

Alisema hivi sasa maofisa biashara hawana idara katika mikoa bali wako chini ya idara ya fedha ambayo wanaisaidia kutafuta mapato.

"Lazima tujenge kada hii na iwe na uwezo wa kufanya kazi. Lazima tuwe na idara ya biashara, hii ndiyo itatusaidia kurahisisha masuala ya uwekezaji kwa kuwa hatuna maofisa uwekezaji sasa lazima tuwageuze nyie ndio mfanye kazi hii," alisisitiza Mwambe.

Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Dk. Maduhu Kazi, alisema lengo la kikao hicho cha siku mbili ni kujifunza na kubadilishana uzoefu katika masuala ya uwekezaji.





# Kilio ukosefu maji ya bomba kubaki historia

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

HATIMAYE kilio cha muda mrefu cha wakazi wa Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya kukosa huduma ya maji ya bomba kitakwisha baada ya serikali kupitia Wizara ya Maji kutenga Sh. bilioni 4.9 kujenga mradi mkubwa wa maji wa Kyela-Kasumulu.

Mbunge wa Jimbo la Kyela, Ally Mlaghila, akiwa bungeni mwaka 2020, aliibua hoja akiiomba serikali kupeleka huduma ya majisafi ya bomba ili kuwasaidia wananchi kuondokana na adha ya muda mrefu ya maji.

Alisema tayari ujenzi wa upanuzi wa chanzo cha maji cha Mbambo umeanza na bomba kuu litakuwa na urefu wa kilomita 107 huku vyanzo vilivyokuwa vikitumika awali vikiendelea kurekebishwa ikiwamo cha Ipinda.

"Kyela imekuwa na kilio cha muda mrefu cha upatikanaji wa majisafi ya bomba, miongoni mwa ahadi zangu kwa wananchi wakati naomba ridhaa ni kuhakikisha huduma ya maji ya bomba inapatikana, tayari utekelezaji umeanza nawahakikishia Wanakyela lazima tuoge maji ya mvua," alisema Mlaghila.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Wilaya ya Kyela, Mhandisi Tanu Deule, alisema wamepokea rola 67 na mabomba 80 kumalizia ujenzi wa mradi wa maji uliopo Kata ya Mababu katika Kijiji cha Kilombero. Alisema mradi huo ni miongoni mwa ambayo serikali kupitia Wizara ya Maji iliwaahidi wananchi kutekeleza ili wananchi wawe na uhakika wa huduma ya maji kuliko ilivyo sasa ambao hutumia maji ya visima.

Alisema mradi wa Mababu utahudumia maeneo mbalimbali ikiwamo Makwale na Matema na kuwaomba wananchi kutunza chanzo hicho.

Vile vile, alisema utekelezaji wa mradi huo na miradi mingine ukiwamo wa Kyela- Kasumulu, utakuwa na tija endapo ushiriki wa wananchi katika utunzaji na ujenzi wa miradi huo utakuwa ni wa moja kwa moja.



Meneja wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Mbeya, Anitha Mshighati (kulia), akiteta jambo na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Nyembea Hamad, wakati wa mafunzo kwa wataalamu wa afya ngazi ya halmashauri ambao watapewa vyeti kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi maeneo ya hospitali, mipakani na maabara, yaliyofanyika mkoani humo juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# TMDA yaagiza ukaguzi maeneo ya utunzaji dawa

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba nchini (TMDA), imewataka wakaguzi wa dawa ngazi ya halmashauri kufanya ukaguzi wa maeneo yanayojihusisha na utunzaji, uuzaji na usambazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi ili kulinda afya za wananchi.

Hayo yalisemwa jana na Meneja wa Kanda, TMDA, Anitha Mshighati, wakati wa mafunzo kwa wafamasia, wataalamu wa maabara na madaktari wa binadamu na mifugo mkoani Songwe.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wataalamu wa kada ya afya waweze kufuatilia ubora wa dawa kwenye masoko pamoja na huduma ya udhibiti ubora ili kuzuia madhara yasiendelee kutokea kwa wananchi.

Alisema washiriki wa mafunzo hayo watapatiwa vyeti kwa ajili ya kufanya shughuli zao za ukaguzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika maeneo yao huku wakipewa nguvu ya kuchukua hatua za kisheria wanapobaini ukiukwaji na uingizwaji wa dawa zikiwamo zilizokwisha muda wake au feki.

"Mna jukumu la kuhakikisha ukaguzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi unafanyika katika vituo vya kutolea huduma za afya, maduka na maabara sambamba na kuchukua hatua za kisheria kwa wanaokiuka sheria ya dawa na vifaa tiba sura ya 219," alisema Mshighati.

Mratibu wa Ofisi za Kanda TMDA, Dk. Henry Irunde, alisema kwa sababu Mkoa wa Songwe unapakana na nchi jirani za Zambia na Malawi ni muhimu wataalamu hao wakaendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo yote ya mipaka na njia za panya ili kuhakikisha bidhaa zinazoingizwa nchini na kusafirishwa nje zinakuwa salama na kukidhi vigezo vinavyotakiwa.

Aliwataka wataalamu hao kuendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara wanaohusika na uuzaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi pamoja na wananchi ili kujiepusha na madhara.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Nyembea Hamad, alizishauri halmashauri zote za mkoa huo kutenga bajeti itakayowawezesha wataalamu wa afya waliopatiwa mafunzo na vyeti kufuatilia na kukagua maeneo yote yanayotoa huduma za dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Alisema kwa kufanya hivyo kutasaidia kudhibiti uuzaji na uingizwaji wa dawa zisizohitajika kwa matumizi ya binadamu.

Aliwashauri wataalamu wa afya kuzingatia miiko na maadili ya kazi zao huku wakijiepusha na vitendo vya rushwa wakati wa kufanya ukaguzi hususani maeneo ya mipakani kama Tunduma.

Alisema Mkoa wa Songwe kwa kushirikiana na TMDA watahakikisha mafunzo waliyopewa wataalamu wa afya yanaleta mabadiliko na kumaliza uuzaji, uingizwaji na matumizi ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

# Waratibu elimu, wakuu wa shule watakiwa ushirikiano

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

SERIKALI wilayani Mbarali, imewataka wenyeviti wa Bodi za Shule za Sekondari, waratibu elimu na wakuu wa shule wilayani humo kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi.

Mkuu wa wilaya hiyo, Reuben Mfune, alitoa kauli hiyo juzi wakati wa kikao cha kujadili namna bora ya kuongeza ufaulu kwa shule za sekondari wilayani humo, kuwa licha ya serikali kuendelea kuboresha miundombinu ya elimu, kikwazo kipo kwa watumishi katika kuongeza ufaulu.

Alisema kikao hicho kilijadili mikakati ya namna ya kuongeza ufaulu kwa kutumia mbinu shirikishi baina ya wanafunzi na walimu kwa kushirikiana na wazazi.

"Tumekaa kikao kazi cha kujadili namna bora ya kuongeza ufaulu miongoni mwa mbinu tunazoona zinafaa ni kuanzisha utaratibu wa wanafunzi kula chakula shuleni, watoto kukaa hosteli na kuanza utaratibu wa masomo ya jioni," alisema Mfune.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Daniel Kamwela, alisema walimu wote watakaokuwa wanafaulisha wanafunzi kwenye masomo wanayofundisha ufaulu wa daraja A na B, watakuwa wanapatiwa zawadi kama motisha na ofisi yake.

Alisema licha ya baadhi ya shule za sekondari kutokufanya vizuri, serikali inaendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu na hadi sasa kuna sekondari 32, kati ya hizo nne ni kwa ajili ya wasichana pekee.

Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Anna Shitindi, alisema wamejipanga kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wote wa shule za sekondari kwa kuhakikisha wanaandaa mitihani ya awali kabla ya mitihani ya taifa.

Alisema wataendelea kuhamasisha wazazi kuchangia chakula shuleni pamoja na kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwa shule zote kubaini dosari zinazojitokeza.





# Waona shida Mahakama Maalum ya Udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WADAU wa kupambana na vitendo vya udhalilishaji kisiwani Pemba wamesema licha ya serikali kuanzisha Mahakama Maalum ya kushughulikia kesi za udhalilishaji Zanzibar, bado kunahitajika nguvu na maboresho zaidi kwenye mahakama hiyo ili kufanya kazi kwa ufanisi na kufanikisha lengo la uanzishwaji wake.

Rai hiyo ilitolewa jana wakati wa mkutano wa wadau kuhusu hatua za utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kupambana na Udhalilishaji ulioambatana na uwasilishaji wa ripoti ya utafiti mdogo wa mwonekano na utendaji wa mahakama maalum ya kushughulikia kesi za udhalilishaji Zanzibar uliofanywa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar.

Said Rashid Hassan kutoka Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar, alisema ili kuondosha usumbufu wa kukosekana kwa mashahidi muhimu, mahakama hiyo iweke mfumo ambao utawezesha wataalamu wote wanaohitajika katika uendeshaji wa kesi hizo, kuwapo mahakamani wakati wote.

"Tutengeneze mahakama ambayo itakuwa inajumuisha wataalamu wote wanaohitajika katika uendeshaji wa kesi za udhalilishaji kama vile madaktari na polisi ili kuepuka hili tatizo la ucheleweshaji wa ushahidi kwa kisingizio cha kukosa ushahidi muhimu ambao unapelekea kesi hizi kucheleweshwa kutolewa hukumu," alisema.

ASP Fakih Yussuf kutoka Dawati la Jinsia la Jeshi la Polisi, alisema ili mahakama hizo zitekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kunahitajia kuwapo mfumo maalum unaowapa fursa maofisa wa dawati wanaosimamia matukio hayo, kuzifuatilia kwa wakati kesi hizo.

"Shughuli za dawati kutokana na umuhimu wake ilitakiwa ipewe kipaumbele maalum kulingana na umuhimu wake na maofisa wanaoshughulikia dawati waachwe wafanye kazi hii tu.

"Sasa hivi unakuta ofisa mmoja huyo anafuatilia matukio ya udhalilishaji, wizi na kesi nyingine kwa wakati mmoja," alisema.

Akiwasilisha mada kuhusu hatua za utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kupambana na Udhalilishaji Zanzibar, Ofisa wa Wanawake na Watoto wilayani Micheweni, Zume Haji Zume, alisema katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Juni, walipokea malalamiko ya wanawake 66 kuhusu matukio mbalimbali ikiwa ni pamoja na migogoro ya ndoa, mimba na mirathi.

"Tumekosa nyumba salama za kuwaweka waathirika baada ya kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji. Hii inapelekea washindwe kutoa ushahidi mahakamani na hii inatokana na kwamba kesi nyingi zinawahusisha wanafamilia na wanapoendelea kukaa pamoja baada ya tukio kutokea, hulishwa maneno ya kukataa kutoa ushahidi," alisema.

Mratibu wa TAMWA Zanzibar, Fat-hiya Mussa Said, alisema utafiti huo umejikita katika kutathmini hatua za utekelezaji wa maagizo ya serikali juu ya uanzishwaji wa mahakama hiyo kwa lengo la kukabiliana na vitendo hivyo katika jamii.

"Malengo ya utafiti huu ni kutaka kuona hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa agizo la Rais katika kuanzisha mahakama maalum ya kushughulikia kesi za udhalilishaji Zanzibar. "Ripoti imebainisha jumla ya matukio 278 yaliripotiwa kwenye vituo vya polisi Unguja na Pemba kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu ambapo katike, 203 ni ubakaji, ulawiti 69 na sita ya kuingilia kinyume na maumbile na kati matukio yote hayo, 244 bado yanaendelea na upelelezi huku 44 pekee yakiwa yanaendelea mahakamani," alifafanua. Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, aliwataka wadau wa kupambana na vitendo hivyo kuendelea kuungana pamoja katika ufuatiliaji wa matukio hayo ili kuhakikisha watoto na wanawake wanabaki salama katika jamii. Alisema utafiti huo utasaidia kutoa mwelekeo wa jinsi ya kukabiliana na matukio hayo ikiwa ni pamoja na kuisadia serikali kufikia malengo ya utekelezaji wa mpango huo.

"Mwelekeo wa kidunia kwa sasa ni kuhakikisha hakuna hata mmoja anayeachwa nyuma katika upatikanaji wa haki, hivyo ili hili lifikiwe, ni lazima kila mmoja kwa nafasi yake kuwajibika ipasavyo," alisema. Mkutano huo ulihudhuriwa na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, mawakili na wajumbe wa mitandao ya kupinga udhalilishaji Pemba.



Mkurugenzi wa Bodi ya Mapato Zanzibar, Salum Yussuf Ali (kulia), akipokea fomu ya ushiriki wa mbio za marathon kutoka kwa mwenyekiti wa mbio hizo, Hassan Zanga, inazotarajiwa kufanyika Julai 18, mwaka huu Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## 'Ushirikiano China, Zanzibar ni imara'

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

BALOZI Mdogo wa China Zanzibar, Zhang Zhisheng, amesema ushirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China utaendelea kuimarika kutokana na udugu wa muda mrefu uliopo.

Alitoa kauli hiyo juzi alipokabidhi msaada wa vifaa tiba kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Dk. Omar Dadi Shajak, huko ofisini kwake Mnazimmoja mjini Zanzibar.

Alisema vifaa hivyo vitasaidia katika utoaji wa huduma mbalimbali ikiwamo barakoa pamoja na mitungi ya hewa ya oksijeni kwa ajili ya Hospitali ya Rufani Mnazimmoja na Hospitali ya Abdalla Mzee iliyoko Pemba.

Balozi huyo alisema ushirikiano unahitajika ili kupambana na wimbi la tatu la Covid-19, ambalo linaonyesha kuathiri duniani kote.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Dk. Omar Dadi Shajak, alimshukuru balozi huyo kwa kuiunga mkono Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuipatia vifaa hivyo pamoja na misaada mingine ikiwamo ya kuwapatia madaktari bingwa.

Aliahidi kuitumia vizuri misaada hiyo ambayo itasaidia katika kupambana na maradhi ya Covid-19 kwa wananchi wa Zanzibar.

Aliwasisitiza wananchi kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya katika kujikinga na maradhi ya corona kwa kuvaa barakoa, kunawa mikono mara kwa mara na kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

Dk. Shajak pia alipokea msaada wa mashine ya kusaidia kupumua kutoka kwa Shirika la Japiego.

# Wizara yajitosa elimu kwa wajasiriamali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhani Soraga, amesema Idara ya Uwezeshaji Kiuchumi ina lengo la kuwapatia elimu na mafunzo wajasiriamali ili kujiongoza katika maisha yao.

Aliyasema hayo Malindi Mjini Zanzibar jana alipofunga shindano la mpango wa biashara kwa wajasiriamali na kuwataka kuendeleza elimu waliyonayo.

Waziri huyo alisema lengo la kupatiwa elimu na mafunzo wajasiriamali hao ni kuwashajihisha kuingia katika ujasiriamali na kuwasaidia kwa kuwawezesha kupata mitaji ili kujiendeleza katika shughuli zao za maisha.

Alisema lengo ni kukuza ubunifu kwa wajasiriamali wadogo na wa kati katika Sekta ya Teknolojia ya Habari (IT), utalii na kilimo ili kutatua shida ya ajira na kuongeza kasi ya mafanikio Zanzibar.

Kutokana na ukosefu wa ajira kwa vijana, alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeweka kituo cha kulea wajasiriamali na kuchukua juhudi katika kubuni nyenzo za miradi tofauti ya kuwawezesha vijana ili kuibua fursa zilizopo katika sekta mbalimbali kwa kuondokana na tatizo la ajira.

Mkurugenzi wa Idara ya Uratibu, Uwezeshaji Kiuchumi, Ameir Haji Sheha, aliwataka wajasiriamali kukuza vipaji vyao ili kujiwezesha kiuchumi na kuacha kuwa tegemezi.

Wajasiriamali wa mafunzo hayo walishukuru serikali kwa jitihada inazozichukua katika kuwawezesha kwa kujiinua kiuchumi ambapo mshindi wa kwanza katika shindano hilo ni Nassor Abdullah Nassor katika mradi wa kugundua gesi 'Rock Tech Service' kati ya washindi 10.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ISSA JUMA BAKARI**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki (King lion) yenye namba ya usajili **MC 798 CBV.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo Cha Polisi. Taarifa ya Polisi

**ARU/KIK/RB/322367/2021**

*116337602*

---

**IIN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**NO.55 OF 2021**
**In the matter of the Estate of the late**
**SARAPIA JEROME MEENA of Maili mbili**
**Mnadani within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of**
**administration by ELIMSAADA E. MEENA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 23rd day of JULY 2021.


**Dated at Dodoma this 29th day of JUNE 2021**

RESIDENT MAGISTRATE

*116338302*

---

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**DAMAS MKELI MBOSA** MWENYE PICHA HAPO JUU AMEPOTEZA PASSPORT YAKE YA KUSAFIRIA YENYE USAJILI NAMBA. **AB669708** ILIYOTOLEWA NA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI (UHAMIAJI) MWAKA **2014**

KWA YEYOTE ATAKAYEIONA AU KUOKOTA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

**POLISI TAARIFA**
**:Rb Namba. MOR/MOR/RB/322649/2021.**

*116337802*

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya mwanzo MAKOLE**
**Usimamizi wa mirathi NA. 63/2021**
**Ombi la MWAJABU HAMISI ALLY kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi Marehemu BARAKA MOHAMEDI**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe **12/07/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 25/06/2021**

Sahihi ya Hakimu

*116338602*

---

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# 130 wafariki dunia kwa joto kali Canada

**British-Columbia,** CANADA

WATU zaidi ya 130 wamefariki dunia kutokana na joto lisilo la kawaida lililovunja rekodi ya kiwango cha joto.

Polisi wa British Columbia, wamepokea taarifa za vifo tangu Jumatatu wiki hii, vingi vikijumuisha wazee.

Walisema kiwango cha joto kupiga katika eneo hilo kilisababisha vifo hivyo na joto liliongezeka zaidi kwa siku ya tatu mfululizo, ilikuwa nyuzijoto 49.5 kijiji cha Lytton, British-Columbia.

Kabla ya wiki hii, kiwango cha joto cha Canada hakikuwahi kuvuka nyuzi joto 45.

"Waangalie majirani zako, familia yako pamoja na wazee unaowajua," Polisi wa Canada Mike Kalanj, ambaye yuko Vancouver Wilaya ya Burnaby, alisema jana.

"Hali ya hewa inaweza kuwa hatari kwa jamii ya watu ambao hawajiwezi hasa wazee na wale wenye matatizo ya kiafya," aliongeza na kuongeza: Ni muhimu tukawajulia hali kila mara.

Kwa mujibu wa polisi, joto hilo linaaminika kuwa limesababisha vifo vya watu 69 katika mji wa Vancouver wilaya ya Burnaby. Wengi wakiwa wazee na waliokuwa na matatizo ya kiafya.

Katika kijiji cha Lytton, mkazi wa eneo hilo Meghan Fandrich alikiambia chombo cha habari cha Globe & Mail kuwa, ilikuwa vigumu hata kutoka nje.

"Hali ilikuwa mbaya sana," alisema na kuongeza kuwa ilimbidi amuhamishe binti yake mdogo kwenda kuishi eneo jingine la British-Columbia ambako joto halikuwa kali sana.

"Tunajaribu kuwa ndani kadiri tuwezavyo. Tumezoea joto lakini si kwa kiwango hiki ambacho kimezidi nyuzi joto 30, ni kingi mno yaani kinafika mpaka 47 hivyo utofauti ni mkubwa sana."

Mamlaka ya Mazingira Canada, ilitoa angalizo juu ya jimbo la British-Columbia na Alberta, pamoja na maeneo ya Saskatchewan, the Northwest Territories na baadhi ya sehemu ya Yukon.

"Taifa letu ni la pili kwa kuwa na baridi duniani na kuwa na barafu," alisema David Phillips, mtaalamu wa mazingira Canada na kuongeza: Tukiongelea suala la joto kuwa kali tunaweza kusema Dubai, lakini hali ya joto tunayoiona hapa ni mbaya zaidi ya Dubai."

Joto katika miji ya Marekani ya Portland na Seattle liliwahi kuvunja rekodi mwaka 1940.

Portland ya Oregon, ilipiga nyuzijoto 46.1C (115F) na Seattle 42.2C (108F), kwa mujibu wa Mamlaka ya Huduma ya Hali ya Hewa. **BBC**



Wakazi wa Jiji la Portland, wakiwa wamejilaza katika jengo lenye viyoyozi ili kupoza miili. Watu zaidi ya 130 wamefariki dunia British Columbia, Canada, kutokana na joto lisilo la kawaida lililovunja rekodi ya kiwango cha joto. **PICHA: BBC**

## Wanaokiuka miongozo ya corona kuchapwa viboko

**Kampala,** UGANDA

WAZIRI wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, Dk. Monica Musenero, ametoa maelekezo kwa Mkuu wa Wilaya ya Butebo, Emmy Mitala, kuwachapa viboko raia watakaokiuka miongozo ya kuzuia maambukizi ya virusi vya corona, Gazeti la Daily Monitor limeandika.

"Wachape tu kama hawasikilizi. Ninatoa maelekezo haya kama mwenyekiti mwenza wa timu ya utekelezaji, usiruhusu watuhangaishe. Nilikuta duka la Petete likiwa limejaa watu, wakiwamo watoto, kama vile hakuna sharti la kusalia nyumbani," alisema Dk. Musenero.

Waziri huyo alitoa maelekezo hayo wakati wa mazishi ya mama mmoja wa miaka 81, Eunice Logose Shaine katika kijiji cha Kabelekeke, mwishoni mwa wiki.

Musenero alilazimika kutoa amri ya kuchapa viboko kwa wakazi hao, baada ya Mkuu huyo wa Wilaya Emmy kulalamika kuhusu kuendelea kukiuka maagizo ya rais, hatua ambayo imeongeza kasi ya kuenea zaidi kwa virusi vya corona, gazeti la Independent limeripoti.

**BBC**

## Wanajeshi 59 waliuawa operesheni Afghanistan

**Kabul,** AFGHANISTAN

UJERUMANI imewaondoa wanajeshi wake wa mwisho Afghanistan na kuhitimisha operesheni zake huku wanajeshi 59 wakipoteza maisha.

Wanajeshi wa mwisho wa Ujerumani katika ujumbe wa Jumuiya ya Kujihami ya NATO, walisafirishwa kwa ndege kutoka kambi ya Mazar-i-Sharif na jeshi la anga la Ujerumani jana, na kuukamilisha ujumbe wake ambao ulianza miaka 20 iliyopita.

Wanajeshi hao walitarajiwa kutua Ujerumani jana.

Waziri wa Ulinzi Annegret Kramp-Karrenbauer alisema ukurasa wa kihistoria umekamilika katika operesheni kali iliyolipa changamoto jeshi la Ujerumani - Bundeswehr na jeshi hilo limedhihirisha umahiri wake katika vita vya Afghanistan.

Kwa mujibu wa Bundeswehr, wanajeshi 59 waliuawa wakati wa operesheni hiyo, wakiwamo 35 katika mashambulizi au vitani.

Aidha Kramp-Karrenbauer alisema Ujerumani inawapa hifadhi wanajeshi wa Afghanistan waliowasaidia Wajerumani kwa mfano wakalimani.

**DW**

## Lyamuremye Jean Claude jela miaka 25 mauaji kimbari

**Kigali,** RWANDA

MAHAKAMA mjini Nyanza Kusini mwa Rwanda, imetoa hukumu ya kifungo cha miaka 25 jela dhidi ya Jean Claude Lyamuremye maarufu 'Nzinga' baada ya kukutwa na hatia ya mauaji ya kimbari.

Jaji wa mahakama hiyo alisema Lyamuremye alishiriki katika mashambulio yaliyofanywa na makundi ya wanamgambo, Intarahamwe katika maeneo mbalimbali mjini Kigali, ambako maelfu ya Watutsi waliuawa.

Lyamuremye mwenye umri wa miaka 46, alijitetea, angeliweza kushiriki mauaji dhidi ya Watutsi kabila la mama yake.

Katika kesi hiyo jana ya kutoa hukumu, mahakama ilisema ushahidi ulionyesha wazi kwamba, wakati wa mauaji ya kimbari, Lyamuremye alikuwa akitembea na silaha mbalimbali pamoja na wanamgambo Intarahamwe kwa lengo la kuwinda na kuwaua Watutsi.

Jaji wa mahakama ya mjini Nyanza, alisema kwamba Lyamuremye alistahili hukumu ya kifungo cha maisha kama ilivyokuwa imependekezwa na mwendesha mashtaka, ingawa kwamba hukumu hiyo ilipunguzwa hadi kifungo cha miaka 25 jela, kutokana na makosa aliyofanya akiwa na umri wa miaka 19 ambao ni umri wa 'kushawishika'.

Kadhalika Jaji alisema pamoja na kuwa alishiriki mashambulio dhidi ya Watutsi na kuna Watutsi wengine aliowasaidia kuokoa maisha yao.

Lyamuremye Jean Claude, alirudishwa Rwanda na nchi ya Uholanzi mwaka wa 2016 ili kukabiliana na mashtaka ya mauaji ya kimbari. Alikamatwa na kuzuiliwa Uholanzi mwaka 2013 alipokuwa dereva wa watumishi wa balozi za Israel na Finland. **BBC**

## Ufaransa yatafakari wimbi la 4 Covid-19

**Paris,** UFARANSA

MSHAURI wa Serikali ya Ufaransa kuhusu Mwenendo wa Virusi vya Corona, Prof. Jean-François Delfraissy, amesema huenda taifa hilo likashuhudia wimbi la nne la maambukizi ya Covid 19.

Amesema ni kutokana na idadi ya juu ya maambukizi inayotokana na virusi aina ya Delta, vilivyotambulika nchini India.

Hata hivyo Delfraissy, aliongeza kuwa kutolewa kwa kasi kwa chanjo ya Covid-19, kunaweza kusaidia kupunguza idadi ya maambukizi na kuzuia wimbi la nne linalotarajiwa Septemba au Oktoba, mwaka huu.

Waziri wa Afya, Olivier Veran mapema wiki hili, alisema virusi aina ya Delta, vimechangia baadhi ya mataifa kutangaza marufuku ya usafiri, vinawakilisha asilimia 20 ya maambukizi ya Covid-19. Ufaransa imesajili visa milioni 182 vya corona pamoja na vifo milioni 3.9.

**RFI**




# RAMOS AFIKIRIA OFA MPYA

**MADRID, Hispania**

SERGIO Ramos ameripotiwa kuwa anajifikiria kukubaliana na ofa kutoka Manchester City, Paris Saint-Germain na Bayern Munich.

Mkataba wa beki huyo na Real Madrid ulimalizika jana na akimaliza muda wake wa miaka 16 katika Uwanja wa Santiago Bernabeu.

Licha ya kuvumilia msimu wa mwisho uliyochanganya sana na Real Madrid, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, anaonekana kunyatiwa na klabu kadhaa za Ulaya.

Kwa mujibu wa ESPN, City, PSG na Bayern zote zimefanya mawasiliano na wawakilishi wa nyota huyo wa Hispania ili kufikia makubaliano.

Ripoti zinaeleza kwamba Ramos sasa anapima kila hatua ya maamuzi, akizingatia mambo kadhaa kabla ya kufikia uamuzi wa mwisho.

Wakati City na PSG wana hamu ya muda mrefu kuwa na mkongwe huyo, Bayern wameingia kwenye mbio za nyota huyo hivi karibuni na Julian Nagelsmann akihitaji kuimarisha safu yake ya beki wa kati.

## FERNANDINHO AONGEZA MKATABA MAN CITY

**MANCHESTER, England**

KIUNGO na nahodha wa Manchester City, Fernandinho Luiz mwenye umri wa miaka 36, amerefusha muda wa kuhudumu kwake pale Etihad baada ya kutia saini mkataba mpya wa mwaka mmoja.

Nyota huyo raia wa Brazil alijiunga na Man City kutoka Shakhtar Donetsk mwaka 2013 na akasaidia miamba hao kushinda mataji manne ya Ligi Kuu England na sita ya ligi.

Fernandinho alikuwa sehemu ya kikosi cha Man City kilichozidiwa ujanja na Chelsea kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Katika fikira zangu, nahisi kwamba kazi kubwa na muhimu zaidi kutoka kwangu nikiwa Man-City bado haijafanyika," alisema mchezaji huyo ambaye mkataba wake wa awali na Man-City ulikuwa umalizike rasmi jana, Juni 30.

"Hiyo ndiyo maana nimeamua kusalia Etihad kwa mwaka mmoja zaidi ili kusaidia klabu kufikia malengo yake."

Man City walimpa Fernandinho unahodha Septemba 2020 baada ya kupendekezwa na idadi kubwa ya wachezaji wenzake hapo Etihad kuwa mrithi wa David Silva aliyetimkia Real Sociedad.



# DE BRUYNE, HAZARD KUIKOSA ITALIA EURO

**MUNICH, Ujerumani**

INGAWA wanasoka Eden Hazard na Kevin de Bruyne watasalia kuwa sehemu ya kikosi cha Ubelgiji kwenye fainali zinazoendelea za Euro 2020, wawili hao watakosa mechi ya robo fainali dhidi ya Italia, kesho.

Nyota hao walipata majeraha yaliyowaweka kwenye ulazima wa kuondolewa uwanjani katika kipindi cha pili katika ushindi wa 1-0 waliopata dhidi ya Ureno kwenye hatua ya 16-bora Juni 27, mwaka huu pale jijini Seville, Hispania.


De Bruyne wa Manchester City alipata jeraha la kifundo cha mguu huku Hazard akipata tatizo la misuli kwenye mguu wake wa kulia.

Kwa mujibu wa kocha Roberto Martinez, wachezaji hao walifanyiwa tathmini na huenda wakarejea kwenye nusu fainali iwapo Ubelgiji watawafunga Italia kwenye robo fainali.

"Majeraha yao si mabaya sana. Hata hivyo, hofu iliyopo kwa sasa ni ufupi wa muda uliosalia kabla ya mechi dhidi ya Italia," alisema Martinez akiwaambia waandishi wa habari.

"Sioni uwezekano wa wao kuwa katika asilimia 100 ya ubora kufikia wakati wa mchezo huu."

Ubelgiji walilazimika kumuachia golikipa, Simon Mignolet kuondoka kambini mwao baada ya kupata jeraha la goti na nafasi yake kuchukuliwa na Thomas Kaminski ambaye sasa ni msaidizi wa Thibaut Courtois anayedakia Real Madrid.



HABARI MICHEZO

# Chelsea yamfuata Pjanic wa Barca

**LONDON,** England

CHELSEA wameripotiwa kushikilia nia ya kumsajili kiungo wa Barcelona, Miralem Pjanic wakati wa usajili huu wa majira ya joto.


Pjanic hakuwa na wakati mzuri katika msimu uliopita pale Camp Nou, akianza katika mechi 13 na 17 akiingia akitokea benchi.

Nyota huyo wa kimataifa wa Bosnia-Herzegovina amebakiza miaka mitatu tu kwenye mkataba wake na Barcelona inatazamia kupunguza bili yao ya mshahara haraka iwezekanavyo baada ya kukubaliana masharti mapya na Lionel Messi.

Kwa mujibu wa Le10Sport, Chelsea sasa iko tayari kushindana na Juventus na Paris Saint-Germain kwa saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31.

Pamoja na Billy Gilmour kuwa ukingoni kujiunga na Norwich City kwa mkopo, kocha wa 'Blues' hao, Thomas Tuchel anahitaji angalau sura mpya katikati ya uwanja.

Ripoti hiyo inaonyesha kuwa makubaliano ya mkopo kwa Pjanic yanauwezekano mkubwa kuliko mkataba wa kudumu.







# Copa America 2020 yatinga robo fainali

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

MICHUANO ya Copa America 2020 sasa imetinga hatua ya robo fainali. Katika Kundi A, Argentina wamefuzu robo fainali wakiwa ndiyo vinara wa kundi hilo wakifuatiwa na Uruguay, Paraguay wakiwa nafasi ya tatu na Chile wamemaliza nafasi ya nne.

Kundi B, Brazil wamemaliza wa kwanza, Peru nafasi ya pili na Colombia wakifuata huku nafasi ya nne ikifungwa na Ecuador.

Hiyo inamaanisha robo fainali itakuwa kama ifuatavyo: Peru vs Paraguay, Brazil vs Chile, Uruguay vs Colombia na Argentina vs Ecuador.

Kwa mantiki hiyo, hatua ya nusu fainali itawakutanisha mshindi wa Peru vs Paraguay atacheza dhidi ya mshindi wa Brazil vs Chile na mshindi kati ya Uruguay vs Colombia atacheza dhidi ya mshindi kati ya Argentina vs Ecuador.

# Low akubali yaishe Ujerumani Euro 2020

**LONDON,** England

KOCHA wa Ujerumani, Joachim Low, amesema kuwa huwa inatokea kwa wachezaji wazuri kutolewa katika hatua ya mtoano kutokana na makosa ambayo wanayafanya, hivyo kwa kilichowatokea kwao hamna namna ya kuzuia.

Katika mchezo wa hatua ya 16 bora ndani ya Euro 2020, Ujerumani ilikubali kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa England.

Raheem Sterling alifunga bao la kwanza dakika ya 75 na lile la pili lilipachikwa na nahodha Harry Kane dakika ya 86, hivyo kuwaondoa wapinzani wao.

England imetinga hatua ya robo fainali ambapo itakutana na Ukraine iliyoshinda mabao 2-1 dhidi ya Sweden.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa England, Gareth Southgate, amesema wachezaji walitumia nguvu nyingi kusaka ushindi mbele ya timu imara jambo ambalo kwao liliwapa matunda.

England imeweza kushinda jumla ya mechi 14 na ililazimisha sare nne huku ikipoteza ushindi katika jumla ya mechi 15 ambazo wamekutana kwenye mashindano yote pamoja na mechi za kirafiki tangu Mei 10, mwaka 1930.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAKIMI KIMEELEWEKA KUSAINI MKATABA PSG

●●● Tumezungumza vitu kadhaa, bado hatuwezi kusema kwamba...

**PARIS,** Ufaransa

WAKALA wa Achraf Hakimi, Alejandro Camano, amesema "wote ambao wanataka kuondoka Inter mara zote wanahuzuni" wakati mlinzi huyo wa pembeni akikaribia kuhamia Paris Saint-Germain.

PSG imeripotiwa kukaribia kukamilisha uhamisho wa Hakimi kwenye Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, licha ya kuwaniwa na mabingwa wa Ligi ya Ulaya, Chelsea.

Baada ya kuwasili kutoka Real Madrid msimu wa 2020-21, Hakimi aliisaidia Inter kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Italia, Scudetto, kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 10, lakini majaliwa yake yamekuwa shakani kutokana na matatizo ya kifedha.

Huku Inter ikijaribu kupunguza gharama kutokana na matatizo ya kifedha baada ya mlipuko wa virusi vya corona, Hakimi ameripotiwa kwamba anatakiwa kuuzwa.

Janga kama hilo pia linaihusu Barcelona na Atletico Madrid, huku wachezaji kama Lautaro Martinez, Romelu Lukaku na Alessandro Bastoni pia wanaweza kuuzwa.

**Camano ambaye amwakilisha Hakimi na Martinez, juzi alieleza majaliwa ya nyota wake hao.**

"Tumezungumza vitu kadhaa, bado hatuwezi kusema kwamba Hakimi ni mchezaji mpya wa PSG," alisema Camano akiiambia Tuttomercatoweb.

"Tumezungumza kuhusu kila kitu.

"Martinez anabaki hapa, kwa sasa yupo na timu ya Argentina kwenye Copa America. Lautaro ni mchezaji wa Inter, ana mkataba wa miaka miwili pale.

"Kama Hakimi ana huzuni kuondoka Inter? Wote wanaoondoka Inter mara zote wanakuwa na huzuni."

Hakimi alicheza mechi 37 kati ya 38 za Inter, akianza kwenye michezo 29.

## KWA UFUPI

**GREALISH AITESA ASTON VILLA**
ASTON Villa wanatumaini watafanikiwa kumzuia nahodha wao, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 25 ambaye anawaniwa na Manchester City. (***Telegraph***)

**RONALDO NA HATIMA JUVE**
JUVENTUS inataraji Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, atafanya uamuzi kuhusu hatima yake ya siku zijazo baada ya Ureno kutolewa kwenye michuano ya Euro 2020. (***Tuttosport***)

**RABIOT ATAKIWA MAN UNITED**
MANCHESTER United ilituma skauti kumchunguza kiungo wa kati wa Ufaransa na Juventus, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 26, huku mabingwa hao wa dunia wakiondolewa katika michuano ya Euro 2020 na Uswisi Jumatatu usiku. (***Star***)

**JUVENTUS WAMTAKA XHAKA**
JUVENTUS imeingia katika ushindani wa kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Arsenal, Granit Xhaka huku klabu ya Roma pia ikidaiwa kuwa na nia ya kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 aliyeiongoza Uswisi kuiondoa Ufaransa katika michuano ya Euro2020. (***Calciomercato***)

**DELANEY AWANIWA DORTMUND**
KLABU za Crystal Palace, Southampton na Norwich City zinamnyatia kiungo wa kati wa Borussia Dortmund raia wa Denmark, Thomas Delaney mwenye umri wa miaka 29, ambaye kandarasi yake inakamilika mwaka 2022. (***Sky Germany***)

**HARRISON KUSAJILIWA RASMI LEEDS**
KIUNGO wa kati wa England, Jack Harrison mwenye umri wa miaka 24, anatarajiwa kukamilisha uhamisho wa kudumu katika klabu ya Leeds United wiki hii baada ya kuhudumu katika klabu hiyo kwa mkopo kutoka Manchester City kwa misimu mitatu. (***Manchester Evening News***)

**LEEDS KUMNG'OA FIRPO BARCA**
LEEDS inatarajiwa kukamilisha usajili wa beki wa Barcelona, Junior Firpo mwenye umri wa miaka 24. (***Goal***)

**RAMSDALE HUYOOO ARSENAL**
ARSENAL inatarajiwa kuwasilisha ofa rasmi kwa golikipa wa Sheffield United, Aaron Ramsdale mwenye umri wa miaka 23. (***Sheffield Star***)

**TUANZEBE KUTUA MAN CITY**
KLABU ya Aston Villa ina nia ya kumsajili beki wa kati wa Manchester City, Axel Tuanzebe kwa mkopo kwa msimu wa 2021-22 huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 akiwahi pia kuichezea Aston Villa kwa mkopo. (***Football Insider***)

**ABRAHAM ASAKWA ASTON VILLA**
ASTON Villa pia inafikiria kumsajili mshambuliaji wa Chelsea na England, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 23, ambaye thamani yake ni pauni milioni 40. (***Eurosport***)

**NEWCASTLE KUTOSAJILI WAZEE**
MMILIKI wa klabu ya Newcastle United, Mike Ashley hayuko tayari kulipa dau la juu kwa wachezaji walio zaidi ya umri wa miaka 27. (***Mail***)



## HABARI MICHEZO

# Edo apania kuipa Mafunzo Kombe la FA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kuukosa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu, Kocha Mkuu wa timu ya Mafunzo, Abdallah Bakar 'Edo', amesema hamu yake kubwa kwa sasa ni kutwaa Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) maarufu FA Cup.

Edo aliyasema hayo juzi baada ya timu yake kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo kwa kuitoa JKU kwa mabao 2-1 katika mchezo wa robo fainali uliopigwa Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

Alisema baada ya timu yake kumaliza nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu Zanzibar msimu huu, nguvu zake na mapambano anayahamishia katika kombe hilo ili kupata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao.

Alisema haoni sababu ya kuukosa ubingwa huo kwa kuwa ana kikosi kizuri na kilichofanya maandalizi mazuri huku kikiundwa na wachezaji wenyewe hamu ya kutwaa makombe likiwamo hilo la FA.

"Tunapambana ili kuhakikisha tunatwaa hili taji na kupata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa, msimu ulioisha tulijipanga kuhakikisha tunatwaa ubingwa wa Ligi Kuu lakini bahati haikuwa yetu licha ya kuweka mipango vizuri, hivyo tunajitahidi na kujipanga zaidi kuweza kupata ubingwa wa FA," alisema.

Mafunzo sasa inafanya jumla ya timu tatu kufuzu hatua ya nusu fainali, ikiungana na KVZ pamoja na Polisi.

# Mtibwa yaipandia Dodoma Jiji Uluguru

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Mohammed Badru, amesema hataki masihara kuelekea mchezo wao dhidi ya Dodoma Jiji FC, baada ya kutumia siku tano za kuwakimbiza wachezaji wake katika milima Uluguru mkoani Morogoro.

Akizungumza na gazeti hili jana, Badru alisema anatumia siku tano hizo kuwafanya wachezaji wake kuwa fiti na baadaye kurudi uwanjani kwa ajili ya kujiandaa dhidi ya mechi ya Dodoma Jiji FC itakayopigwa Julai 14, mwaka huu katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Alisema wanahitaji kupata matokeo mazuri katika mchezo huo kwa lengo la kujiweka katika mazingira mazuri ya kuendelea kubaki Ligi Kuu kwa msimu ujao.

"Tuna mechi mbili mkononi, zote tunatakiwa kushinda, hivyo hatuna muda wa kupumzika, nimetenga siku tano kwa ajili ya mazoezi katika milima na baadaye tutarudi uwanjani kwa ajili ya kimbinu na kiufundi," alisema Badru.

# MBIO ROCK CITY MARATHON 2021 ZAZINDULIWA MWANZA

**Na Mwandishi Wetu**

MSIMU wa 12 wa Mbio za Rock City Marathon, zinazofanyika kila mwaka jijini Mwanza, umezinduliwa rasmi jana jijini humo huku serikali ikiahidi kuendelea kutumia mbio hizo kuibua vipaji vya mchezo wa riadha sambamba na kutangaza utalii wa ndani.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi huo, Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Elias Masala, aliyekuwa akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Robert Gabriel, alisema ni nia ya serikali kuona mashindano hayo yanakuwa chachu ya kuwezesha kupatikana wanamichezo watakaoweza kushiriki katika mashindano ya kitaifa na kimataifa.

"Ili agenda kuu ya kutangaza utalii wetu iweze kufanikiwa, ni wazi kwamba lazima tuwe na matukio yanayoweza kuwashawishi wenzetu kutoka nje waje kututembelea. Uwapo wa mashindano makubwa kama haya ndio utatuwezesha kufanikisha hili, hivyo nawasihi wadau wote tujitokeze kuunga mkono mbio hizi," alisema Masala, ambaye aliahidi kushiriki mbio hizo.

Mbio hizo zinazotarajiwa kufanyika Oktoba 24, mwaka huu kwenye viunga vya jengo la Biashara la Rock City Mall, jijini Mwanza na tayari zimefanikiwa kuvutia wadhamini na wadau mbalimbali ikiwamo Kampuni ya TIPER, Serengeti Breweries, Benki ya KCB, Kampuni ya Uhandisi ya Magare, Pepsi, Maji ya Uhai, Rock City Mall, Kampuni ya Ulinzi ya GardaWorld, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Azam TV na CF Hospital.

Zaidi Msala alitoa wito kwa wadau na wakazi kutoka ndani na nje ya jiji hilo kuhakikisha wanashiriki katika matukio mbalimbali yatakayoambatana na mbio hizo ikiwamo kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo Kanda ya Ziwa, kushiriki mbio zenyewe pamoja na kuwa sehemu ya wadhamini wa mashindano hayo.

**Kwa upande wa Mratibu wa mbio hizo kutoka Kampuni ya Capital Plus International, Kasara Naftal, alisema maandalizi yanaendelea vizuri huku akibainisha kuwa lengo haswa ni kushirikisha washiriki zaidi ya 5,000.**

"Tunajitahidi kufanya maandalizi ya kutosha na yenye kufuata viwango vya kimataifa ili kuwawezesha washiriki wa mbio hizi wakiwamo wale wa kimataifa wapate wasaa wa kushiriki kikamilifu bila vikwazo vya aina yoyote.

"Hili pia huwa tunalifanya makusudi ili washiriki hawa wakawe mabalozi wazuri wa mbio hizi pamoja na malengo ya kuanzishwa kwake kwa maana ya kutangaza utalii pindi wanaporudi katika mikoa na mataifa yao hasa kwa wale wanaotoka nje ya nchi," alisema.

Mbali na mbio za Km. 21, Mbio za Rock City Marathon pia zinatarajiwa kuhusisha makundi mengine ya mbio ambayo ni pamoja na mbio za Kilomita 10 kwa wanaume na wanawake, Kilomita tano kwa ngazi ya 'corporate' na watu wenye ualbino pamoja na watoto wenye umri kuanzia miaka saba.

Kuhusu usajili wa mbio hizo, Naftal alisema unatarajiwa kuanza rasmi leo kwa njia ya mtandao.




Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Elias Masala (aliyeshika mkasi), akikata utepe kuashiria uzinduzi wa msimu wa 12 wa Mbio za Rock City Marathon zinazotarajiwa kufanyika Oktoba 24, mwaka huu, kwenye viunga vya jengo la Biashara la Rock City Mall, jijini Mwanza wakati wa hafla maalum ya uzinduzi wa mbio hizo iliyofanyika jana. Wanaoshuhudia ni wadau mbalimbali wa mbio hizo wakiwamo viongozi wa serikali, viongozi wa mchezo huo, wadhamini na waandaaji wa mbio hizo. **MPIGAPICHA WETU**

# Rage: Mchakato uchaguzi TFF uko sawa

**Na Adam Fungamwango**

KATIBU Mkuu wa zamani wa Chama cha Soka Tanzania (FAT) kwa sasa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Ismail Aden Rage, amesema mchakato wote wa uchaguzi wa shirikisho hilo, umefanyika kwa kufuata taratibu zote za sheria na kanuni, tofauti na baadhi ya watu wanavyolalamika.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Rage alisema kuwa amesoma sheria zote za uchaguzi na kanuni zake na hajaona hata sehemu moja ambayo imepindishwa au kusiginwa.

Juzi, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Benjamin Kalume, alitangaza uamuzi wa kamati hiyo kumpitisha Wallace Karia anayetetea nafasi yake kwenye kiti cha Urais wa TFF akiwa mgombea pekee baada ya wagombea wawili waliobaki kwenye awamu ya pili, Hawa Mninga na Evance Mgeusa, kuenguliwa kwa vigezo vya kukosa sifa.

"Mimi nimesoma sheria na kanuni zote za uchaguzi, kamati iko sahihi kabisa. Hawajakosea, na nimeona hata wagombea wenyewe wamekiri na kukubali," alisema Rage.

Kiongozi huyo aliwataka watu wanaotaka kugombea uongozi kuwa wale ambao wameshawahi kucheza soka, au kuongoza klabu mbalimbali na si kila mtu tu anaweza kuongoza taasisi hiyo kubwa ya soka nchini.

"Kuongoza soka ni kazi ngumu. Sisi tumepita pale, tunajua hilo. Huwezi kutoka tu huko na kuwa kiongozi wa soka, kwa hiyo nawashauri wawe wanajipanga kweli," alisema.

Aliongeza kuwa kati ya wagombea wote ambao walijitokeza safari hii, mtu ambaye alikuwa ana uwezo wa kumtikisa Karia ni mwanasoka wa zamani wa Yanga na Taifa Stars, Ally Mayay.

"Yule alikuwa na uwezo wa kuongoza, lakini kwa bahati mbaya alishindwa mwanzoni. Na Kamati ilikuwa sawa tu tangu mwanzoni, kwani ilikuwa ikifanya hivyo kutokana na kanuni zilizopitishwa na wajumbe wenyewe," alisema.

Kwenye mchujo wa kwanza, Mayay, Ally Saleh na Oscar Oscar walienguliwa kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kushindwa kufikia idadi ya wadhamini waliotakiwa.

Michezo
Alhamisi Julai 1, 2021
Nipashe



HAKIMI KIMEELEWEKA KUSAINI MKATABA PSG HABARI UK 22

CHA KWANZA...



Mshambuliaji wa England, Raheem Sterling, akiifungia timu yake bao la kwanza wakati ikishinda 2-0 dhidi ya Ujerumani kwenye mechi ya hatua ya 16-bora ya michuano ya Euro 2020 iliyopigwa Uwanja wa Wembley juzi. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YATISHWA NA MORRISON, MIQUISSONE

●●●Simba yaiambia tatu bila hazikwepeki Jumamosi, Waziri Mkuu afunga Bunge akizitaja...

**Saada Akida na Augusta Njoji**

KUELEKEA mechi ya watani wa jadi Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, wenyeji wa mchezo huo wa Ligi Kuu Bara, Simba wamesema kama waamuzi wakitumia sheria 17 za soka ipasavyo bila kuzipindisha, wanaamini hakuna kitakachowazuia kushinda mabao 3-0.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, alisema mchezo huo mkubwa ambao unakutanisha miamba miwili ya soka nchini, ni muhimu kwao kwa sababu wakipata pointi tatu watakuwa wametangazwa kuwa mabingwa kwa mara ya nne mfululizo na kama wakitoa sare watakuwa mabingwa wateule.

"Waamuzi wakichezesha kwa haki na kufuata sheria tukiwa na Miquissone (Luis), Morrison (Bernard), Bocco (John), Chama (Clatous), Wawa (Pascal), wakiwa fiti hawa wachezaji wetu wote ninaamini Yanga hawatoki si chini ya mabao 3-0 katika mchezo huo," alisema.

Alisema dhamira ya Simba ni furaha, mbali na kuwekeza katika maendeleo ya soka, ni kuwapa raha mashabiki wao kwa kuhakikisha kila Mwanasimba anapata furaha katika mechi zao zote zilizobaki za ligi hiyo.

"Niwaombe mashabiki Jumamosi tuvae jezi zetu ndani na juu makoti na tutakaposhinda basi wasiondoke uwanjani wasubiri kwa dakika tano ili kuwapigia makofi wachezaji wetu kwa ishara ya kuwapongeza kwa kutwaa ubingwa," alisema Manara.

Ofisa habari huyo aliweka wazi kuhusu tetesi za Miquissone kutajwa kuwa msimu ujao huenda akatimkia Yanga, kwamba nyota huyo bado ni mchezaji halali wa Simba kwa sababu bado ana mkataba.

"Hizo ni taarifa za uchochezi na kutaka kututoa katika mwelekeo wa mechi yetu ya Jumamosi, mashabiki watambue kwamba nyota huyo ana mkataba na Simba kama kuna timu inamhitaji basi inatakiwa kutoa Dola milioni 10," alisema. Manara alisema licha ya kuwa kimya katika kusajili tayari uongozi wa timu hiyo imewasajili nyota watatu wa kigeni kwa ajili ya msimu ujao kulingana na mahitaji ya benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Mfaransa Didier Gomes.

"Simba huwa hatufanyi mambo kwa ajili ya sifa kama ilivyo kwa wenzetu, niwape hili kwamba tayari tumewasajili wachezaji wapya watatu (hakuweka wazi majina na nchini wanazotoka), hakuna yeyote anayejua, hivyo ikifika muda kila kitu kitakuwa wazi, katika hilo mashabiki wasiwe na hofu na kutakiwa kujitokeza uwanjani kwa wingi Jumamosi," alisema Manara.

Meneja Biashara wa N-Card , Jackson Jaka, alisema mashabiki waliokata tiketi katika mchezo huo ulioahirishwa wa Mei 5, mwaka huu, wamerudishiwa kadi zao hivyo wanatakiwa kufika nazo uwanjani kwa ajili ya kuhakiki na kuingia uwanjani kushuhudia mechi hiyo.

Kwa upande wa Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema: "Maandalizi yanaendelea vizuri kama kawaida, kikosi chetu kinazidi kuimarika kila siku na sitaki kuongea sana, lakini mtajionea wenyewe kinachoenda kutokea."

Katika hatua nyingine wakati akisoma hotuba ya kuahirisha bunge jijini Dodoma jana, Waziri Mkuu wa Tanzania, Kassim Majaliwa, alisema Jumamosi ni siku inayongojwa kwa hamu na wanamichezo nchini hasa wapenzi wa soka"Siku hiyo vigogo wawili wa soka nchini watapambana katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. Tunazitakia ushindi timu zote," alisema.

## RAGE AFUNGUKA KARIA MGOMBEA PEKEE TFF



**Na Adam Fungamwango**

KATIBU Mkuu wa zamani wa Chama cha Soka Tanzania (FAT) kwa sasa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Ismail Aden Rage, amesema mchakato wote wa uchaguzi wa shirikisho hilo, umefanyika kwa kufuata taratibu zote za sheria na kanuni, tofauti na baadhi ya watu wanavyolalamika.

UK. 23

## RAMOS AFIKIRIA OFA MPYA BAYERN, CITY

**MADRID, Hispania**

SERGIO Ramos ameripotiwa kuwa anajifikiria kukubalina na ofa kutoka Manchester City, Paris Saint-Germain na Bayern Munich.

UK. 20

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002